# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatano Oktoba 14, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580368

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


**MATATANI** tuhuma za kumpiga mpenzi wake risasi wivu wa mapenzi

UKURASA 3



**TUNDU** Lissu aahidi kupandisha mishahara watumishi wa umma

UKURASA 7




UKURASA 11

# BALAA

**MVUA** yaibua hofu Dar, nyumba, magari vyazama, barabara zageuka majaruba, TMA yasisitiza bado ipo... *Endelea Uk. 2*



Baadhi ya wakazi wa Kitunda Kivule, jijini Da es Salaam, wakipanda ngazi kuvuka upande wa pili wa Mto Kerezange, baada ya barabara ya muda kukatika kutokana na mvua kubwa iliyonyesha jana. Picha zaidi Uk. 19. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## KUMRADHI

JPM: Tanzania ina maadui wa rasilimali

UKURASA 2

# JPM apokea gawio bil. 100/- mapato dhahabu

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA YATABIRIWA KUFIKA FAINALI MABINGWA AFRIKA UK. 23

MAONI, KATUNI UK. 6


Fursa kwa Wagombea! 2020

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote walioptishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kuidishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

# Mvua yazua balaa Dar

**Na Romana Mallya**

NI balaa! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na madhara ya mvua kubwa iliyonyesha jana Dar es Salaam na kusababisha mafuriko kwenye miundombinu ya barabara na makazi ya jiji hilo la kibiashara.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), aliiambia Nipashe jana kwamba, mvua hiyo inatarajiwa kuendelea kunyesha kwa viwango tofauti kwa siku tatu mfululizo kuanzia jana na kuwataka wananchi kufuatilia utabiri wa mamlaka hiyo.

Dk. Agnes Kijazi alisema mvua hiyo kubwa inayonyesha Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Morogoro kwa kipindi ambacho siyo kawaida mikoa hiyo kupata mvua kubwa, inatokana na mabadiliko yaliyotokea.

"Leo (jana) tumeona mvua imenyesha kwa wingi na kuna wingu zito katika maeneo ya Dar es Salaam ila kesho (leo) tunategemea kuwa na upungufu kiasi na keshokutwa (Alhamis) itaendelea kuwapo na baada ya hapo itakatika," alisema.

Alisema mvua hiyo inayoendelea kunyesha imekuja kama walivyotabiri na kuwataka wananchi, hasa wanaokaa bondeni, kuchukua tahadhari.

"Wito wetu kwa wananchi waendelee kufuatilia taarifa zetu tunazozitoa kwa sababu tumeonyesha katika msimu huu tutakuwa na mvua ambayo ni ya chini ya wastani na inaweza kujitokeza siku chache ambazo itanyesha mvua kubwa na kuleta mafuriko.

"Tunashauri wananchi wafuatilie utabiri tunaotoa kila siku, utabiri wa jana (juzi) tulisema kutakuwa na mvua kubwa itakayokuwa na ngurumo na itakuwa kubwa jijini Dar es Salaam na ndivyo ilivyojitokeza," alisema.

MAFURIKO DAR

Baadhi ya barabara za Jiji la Dar es Salaam jana zilijaa maji na kusababisha foleni kubwa ikiwamo ya New Bagamoyo ambayo iko katika ujenzi wa upanuzi.

Nipashe ilishuhudia usumbufu mkubwa wa watumiaji wa barabara katika kipande cha Mwenge-Bamaga ambacho mkandarasi anaendelea na ujenzi, kikiwa kimejaa maji na kusababisha foleni kubwa kwa watumiaji wa barabara hiyo.

Maeneo mengine ambayo watumiaji wa barabara walipata usumbufu ni pamoja na Jangwani ambako mradi wa mabasi yaendayo haraka umepita.

Mvua hiyo iliyoanza alfajiri, iliathiri pia barabara zinazopita maeneo ya Mbezi Beach na Mbezi Chini ambazo hutumiwa na wananchi wanaotoka Tegeta kwenda mjini.

Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alisema jana kuwa, wamelazimika kuifunga Barabara ya Morogoro eneo la Jangwani kutokana na maji kupita juu ya daraja na kusambaa maeneo hayo.

"Barabara nyingine ambazo zimepata madhara ya maji kupita juu ni za Kawawa na Kigogo, mpaka sasa (jana jioni), hakuna athari zozote kwa binadamu zilizoripotiwa polisi kuhusiana na mvua hii inayoendelea kunyesha," alisema.

Kamanda Mambosasa alitoa wito kwa wananchi, hasa wanaokaa bondeni, wachukue tahadhari ya kuhama kwa muda maeneo hayo kwa sababu mvua hiyo inaendelea.

## KUMRADHI

### JPM: Tanzania ina maadui wa rasilimali

KATIKA toleo letu la jana ukurasa wa mbele, habari kubwa iliyokuwa na kichwa cha habari 'JPM asema Tanzania ina maadui wengi wa nje' ilimnukuu vibaya na kusababisha usumbufu kwa nchi marafiki na wasomaji kwa ujumla.

Usahihi wa habari hiyo ni kuwa mgombea urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, alisema hatua alizozichukua ikiwamo kudhibiti utoroshaji madini kumeifanya Tanzania kujitengenezea maadui wa rasilimali.

Alizungumza hayo juzi kwenye kampeni za uchaguzi mkuu, wakati akiomba kura kwa wakazi wa Wilaya ya Ilala eneo la Kinyerezi.

Alisema hatua za kujenga ukuta katika mgodi wa mirerani, pamoja na kudhibiti usafirishaji wa makinikia, kumesababisha yeye (Rais Magufuli) kuchukiwa.

Alisema: "Ndugu zangu tumejitengenezea maadui. Hatua tunazozichukua haziwafurahishi watu. Ujenzi wa ukuta Mirerani, usitishwaji wa usafirishaji wa makinikia, ujenzi wa bwana la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere, kuishinda corona, hawawezi kufurahi, lazima watuchukie kwa sababu walitaka kuigeuza Tanzania sehemu ya kuchuma".


Dk. Magufuli alisema awali madini ya Tanzanite yalikuwa yanasombwa usiku na mchana na kusafirishwa kwenda nje ya nchi, huku Tanzania ikibakiwa na mshimo na kutoambulia chochote.

Alisema Tanzania haikuwa katika nafasi ya kwanza wala ya pili wala ya tatu kwa uuzaji wa madini ya Tanzanite duniani, licha ya madini hayo kupatikana pekee hapa nchini.

"Nilipoingia madarakani nikaanza kujenga ukuta eneo lote la uchimbaji, watu wakaanza kunishangaa, lakini leo faida tunapata, tumefunga 'camera' tuna 'monitor' (uangalizi) na akina Laizer leo wamepatikana. Hao watu hawezi kufurahi lazima watuchukie sisi".

Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote uliojitokeza.

**Mhariri**




Rais John Magufuli akipokea gawio la Sh. bilioni 1.1 kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Meja Jenerali mstaafu, Michael Isamuhyo na wajumbe wa bodi hiyo, wakati wa hafla ya kupokea gawio toka kwa kampuni ya madini ya TWIGA na Shirika la Madini la Taifa STAMICO, jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (wa pili kulia) na Msajili wa Hazina, Athumani Mbuttuka. **PICHA: IKULU**

# JPM apokea gawio bil. 100/- mapato dhahabu

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imepokea gawio la Dola za Marekani milioni 40 (Sawa na Sh. bilioni 100) kutoka kampuni ya Twiga, huku Rais John Magufuli akiwakaribisha wawekezaji zaidi kutoka nje kuja kuwekeza nchini.

Akizungumza wakati wa halfa ya kupokea gawio hilo jana jijini Dar es Salaam, Rais Magufuli alisema gawio hilo limetokana na serikali kumiliki asilimia 16 ya hisa kutoka kampuni ya uchimbaji madini ya Barick, huku asilimia 84 zikimilikiwa na kampuni hiyo.

Rais Magufuli alisema kuna baadhi ya watu walikuwa wanabeza mazungumzo yaliyofanyika miaka ya nyuma kati ya Serikali na Kampuni ya Barick.

Alisema gawio hilo liwe fundisho kwa watu waliokuwa wanapinga kwamba ni muda mwafaka kwao kuanza kutubu kwa viongozi wa dini.

"Mimi huwa naamini na siogopi kuwa sadaka kwa Watanzania. Kwa muda huu mimi ndiye rais, nitaendelea kusimamia maslahi ya Watanzania hadi pale atakapopatikana rais mwingine. Nataka Watanzania masikini wanufaike na rasilimali za nchi yao," alisema.

Alisema gawio hilo litakwenda kutumika katika kuendeleza sera ya elimu bure, ujenzi wa barabara, hospitali, huduma za kijamii, kununua vifaa vya operesheni na kuokoa vifo vya mama wakati wa kujifungua.

"Nitumie fursa hii kuwakaribisha wawekezaji wa nje na wa ndani kuja kuwekeza hapa nchini, serikali haichukii wawekezaji bali tunahitaji faida ya usawa siyo wa kutuachia mashimo. Ninaimani Barick watakuwa mabalozi wazuri wa kueleza Tanzania ni sehemu salama kwa uwekezaji," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Tunawakaribisha wawekezaji kwenye gesi, mafuta, dhahabu, mtu yeyote aje atoke Tanga, Mtwara, Vietinam au China, Marekani, 'The room is open' (mazungumzo yapo wazi). Tunataka kufanya biashara, tunataka kujenga uchumi, hii ndiyo Tanzania tunayoitaka," alisema Rais Magufuli.

Alisema Tanzania ina utajiri mkubwa wa madin, na kwamba jitihada kubwa zimefanyika katika kuijenga sekta ya madini.

Alisema awali udhibiti kwenye madini ulikuwa ni mdogo, wizi ulishamiri sambamba na utoroshaji wa madini na ukosekanaji wa masoko.

"Mchango wa sekta ya madini kwenye pato la taifa limeongezeka kutoka asilimia 3.4 mwaka 2015 hadi 5.2 mwaka 2019/20, pamoja na kuongeza upatikanaji wa ajira kutoka milioni moja hadi milioni 1.5," alisema.

Mbali na serikali kupokea gawio hilo, pia ilipokea Sh. bilioni 1.1 kutoka kampuni ya Stamico.

Naye Waziri wa Nishati, Doto Biteko alisema jitihada za serikali katika kuinua sekta ya madini umekuwa mkubwa tangu mwaka 2015.

Alisema mashine za ukataji madini zimeongezeka kutoka 120 zilizokuwapo mwaka 2015 hadi 560 mwaka huu, alisema serikali imeweza kuanzisha masoko 38 nchini pamoja na vituo 37 vya kununua madini.

Biteko alisema: "Mwaka 2015 sekta hii ilikuwa nyuma sana, ilijaa uficho na usiri mkubwa, Rais Magufuli alipoingia madarakani alirekebisha sheria, mapato yakaanza kuongezeka".

# HABARI KITAIFA

## Adaiwa kumpiga risasi mpenzi wake kisa wivu wa mapenzi

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma, linamshikilia fundi ujenzi Daniel Massawe, maarufu kwa jina la Madevu (40), mkazi wa Kisasa, kwa tuhuma za kumjeruhi kwa risasi mpenzi wake kwa madai ya wivu wa mapenzi.

Binti huyo ambaye jina lake limehifadhiwa hivi sasa amelazwa kwenye chumba cha wagonjwa wa uangalizi maalum (ICU) katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, akiendelea na matibabu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Gilles Muroto, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa jana baada kumjeruhi binti huyo.

Alisema mtuhumiwa alikamatwa akiwa na bastola aina ya Browing Calb 7.65 Maker namba A 748082, CAR namba 95632 ikiwa na risasi saba kinyume cha sheria na kuitumia katika uhalifu na kuhatarisha maisha ya watu wengine.

"Uchunguzi unaendelea kubaini silaha hiyo ameipataje na atafikishwa mahakamani mara upelelezi ukikamilika. Hakuna mhalifu atakayebaki salama, uhalifu haulipi na kila mtu azingatie utii wa sheria kwa kufanya kazi halali," alisema.

Katika hatua nyingine, Kamanda Muroto alisema wanamshikilia Mkazi wa Kijiji cha Ikengwa Wilaya ya Kondoa, Nzara Simon (21) kwa tuhuma za kukutwa na meno mawili ya tembo ambayo ni nyara ya serikali kinyume cha sheria.

Alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 11, mwaka huu, na mtuhumiwa atafikishwa mahakamani huku wakiendelea na msako mkali wa kuwatafuta watuhumiwa wengine.

Pia alisema wanawashikilia watuhumiwa watatu kwa tuhuma za kukutwa na vipande viwili vya meno ya tembo katika kijiji cha Chaludewa wilayani Mpwapwa.

Kamanda Muroto aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Nchemba Masonga (75) mkazi wa Chaludewa, Sanyiwa Nkubha (38) mkazi wa kijiji cha Chiboli wilayani Mpwapwa na Daudi Nhimko (48) mkazi wa Gairo.

Wakati huo huo, jeshi hilo linawashikilia watu watatu kwa kukutwa na silaha ya kivita aina ya AK 47 yenye namba UR 2716 ikiwa na risasi 27 ambayo walikuwa wakiitumia kufanya ujangili.

Aliwataja watuhumiwa waliokatwa kuwa ni Mngoya Juma (40), Amrani Mohammed (34) na Furaha Masaka (20) ambao wote ni wakazi wa Banyibanyi wilayani Kongwa.

## Chanzo moto Mlima Kilimanjaro hiki hapa

**Na Mary Mosha, MOSHI**

UCHUNGUZI wa awali wa vyombo vya usalama kuhusu moto mkubwa uliozuka katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, umebaini baadhi ya wapishi waliokuwa na makundi ya watalii, waliwasha moto kupasha chakula na kushindwa kuuzima kikamilifu.

Moto huo ulizuka Oktoba 11 mwaka huu katika eneo la Whona, ambacho ni kituo cha kupumzika wageni wanaotumia njia ya Mandara na Horombo.

Jana, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), anayeshughulikia mawasilino, Paschal Shelutete, alisema wapishi hao baada ya kumaliza kupasha chakula kwa ajili ya watalii, kwa bahati mbaya walisahau kuuzima na moto huo kushika kwenye nyasi.

"Jitihada zinaendelea kuhakikisha moto huo unazimwa kwa kutumia vikosi mbalimbali vikiwamo vya Zimamoto na Uokoaji, wanafunzi wa Chuo cha Kimataifa cha Usimamizi na Uhifadhi a Wanyamapori-Mweka, wananchi kutoka vijiji jirani na jeshi la akiba.

"Chanzo cha moto huu mpaka sasa hivi pamoja na kwamba uchunguzi unaendelea, kulikuwa na wapishi wakipasha moto chakula. Kwa bahati mbaya wapishi walisahau moto huo na kushika kwenye nyasi na kuleta madhara haya," alisema.

Shelutete alisema TANAPA bado inaendeela na uchunguzi wa kina, akisisitiza kuwa shirika hilo linaona tukio hilo ni la bahati mbaya na halikutarajiwa kutokea.

Kwa mujibu wa Shelutete, jitihada za kuuzima moto huo bado zinaendelea, akibainisha kuwapo kwa mafanikio makubwa katika jitihada za kuudhibiti.

Hata hivyo, Shelutete alisema moto huo uliwazidi nguvu majira ya usiku na kusambaa kwa kasi zaidi kutokana na upepo mkali unaovuma.

"Jitihada zinaendelea kuhakikisha moto huo unazimwa kwa kutumia vikosi mbalimbali vikiwamo vya Zimamoto, wanafunzi wa Mweka, wananchi wa vijiji jirani pamoja na jeshi la akiba," alisema.

Shelutete alisema moto huo kwa jana ulikuwa kwenye uelekeo wa kwenda Kituo cha Horombo ukitokea Kituo cha Mandara.

"Njia zote wanazopandia wageni, tunazipa kipaumbele kiusalama kuhakikisha kwamba wageni wanakuwa salama na shughuli zote za utalii zinaendelea kama kawaida, hivyo niwatoe hofu watalii waendeele kuja na kufurahia mandhari ya mlima wetu," alisema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana, baadhi ya viongozi wa vijiji vya jirani, akiwamo Herry Temu ambaye Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kitowo, alitoa wito kwa watu wengine kujitokeza kushiriki katika uzimaji wa moto ili kuokoa mlima huo.

Dmitry litkor, mtalii kutoka Hispania, akieleza hisia zake kuhusiana na moto huo, alisema licha ya kuwapo kwa moto, wamefanikiwa kufika Kilele cha Uhuru.

"Jana (juzi) mchana, tulisikia harufu ya Moshi, lakini wahudumu wa hifadhi hii pamoja na waongoza watalii, walitusaidia na tumerudi salama bila madhara yoyote," alisema Denis Romonov, mtalii mwingine kutoka Denmark.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - IKULU

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII



Julius Kambarage Nyerere
(1922 - 1999)

KUMBUKUMBU YA MIAKA 21 YA KIFO CHA **BABA** WA **TAIFA**,
MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE

Mwenyekiti, Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF wanaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, na Watanzania wote katika kumbukumbu ya miaka **21** ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere

TASAF itaendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano katika kupambana na umaskini kama ishara ya kuenzi mchango wa Mwalimu Nyerere dhidi ya umaskini.

***Pamoja Tuondoe Umaskini***

Mkurugenzi Mtendaji
**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF**
S.L.P. 2719 Dodoma, Tanzania
Simu: **+255 26 296 3866** Nukushi: +255 26 296 3871
Tovuti: **www.tasaf.go.tz** Barua pepe: **info@tasaf.go.tz**

215941302



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akiwaonyesha waandishi wa habari jijini Dodoma jana, silaha ya kivita AK 47 yenye namba UR 2716 ikiwa na risasi 27, iliyokamatwa katika kijiji cha Banyibanyi wilayani Kongwa ikidaiwa kutumika katika uhalifu wa ujangili. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# JPM afuta ushuru 'Mahakama ya Ndizi'

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli ameamuru soko la ndizi la Mabibo, maarufu kama 'Mahakama ya Ndizi' kubaki chini ya wananchi wanaofanya biashara katika eneo hilo, sambamba na kutolipa ushuru.

Alisema wafanyabiashara katika soko hilo watakapokuwa na vitambulisho vya ujasiriamali, hawatalazimika kulipa tena ushuru waliokuwa wanatozwa tangu awali.

Magufuli ambaye ni mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), alitoa kauli hiyo jana katika Uwanja wa Barafu Mburahati, wakati akiwahutubia wananchi na wanachama wa CCM, waliojitokeza kumsikiliza akiomba kura kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

"Natamka leo (jana) kwa heshima mliyonionyesha ya kunisubiri kwenye mvua. Kwa mamlaka niliyonayo, soko hili litabaki kuwa chini ya wananchi wa hapo wafanyabiashara. Kama patakuwa na utaratibu mwingine, kuanzia leo (jana) wanaofanya biashara katika soko hilo hakuna kutozwa ushuru bali watalipia vitambulisho," alisema.

Rais Magufuli alisema waliokuwa viongozi wa jimbo la Ubungo hawakushughulikia tatizo hilo, hivyo kwa sasa ni wakati mwafaka kwa wafanyabiashara hao kufanya shughuli zao bila ya kubugudhiwa.

**AWASHUKURU WANANCHI**

Aidha, Rais Magufuli aliwashukuru wananchi wa Jimbo la Ubungo kwa hatua ya kujitokeza kwa wingi, wakinyeshewa mvua bila ya kuondoka wakati akihutubia na kabla ya kufika kwake.

"Sijawahi kuhutubia mkutano wa hadhara wananchi bila ya kujali mvua wananisubiri mimi. Ni upendo wa hali ya juu. Mmeniachia deni kubwa. Sijawahi kuona upendo huu, kweli nimeguswa, sijui niwafanyie nini, niwalipe nini, sijui nianze na soko la Mahakama ya Ndizi?," alisema.

Rais Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano ya utawala wake serikali ilipokuwa inaidhinisha pesa za miradi ya maendeleo katika Jimbo la Ubungo zilikuwa hazitumiki kama zilipopangwa.

Alisema miradi mingi ilikuwa haiendi kama ilivyotakuwa kulikosababishwa na baadhi ya viongozi wa upinzani waliokuwa wanaongoza jimbo hilo.

**YALIYOFANYIKA**

Rais Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano ya utawala wake mambo mengi yamefanyika katika Jimbo la Ubungo, ikiwamo ujenzi wa miradi mikubwa miwili ya maji.

Alisema mradi wa kwanza ni kutoka Mlandizi hadi Kibamba uliogharimu Sh.bilioni 94.9, mwingine ni Ruvu Chini kupitia Bagamoyo hadi Chuo Kikuu, kwa gharama ya Sh. bilioni 131.4.

"Miradi hiyo imesaidia upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam, siku hizo malori ya kuuza maji yamepungua, siku hizi yanatangatanga kutafuta wateja na siyo wateja kutangatanga," alisema Rais Magufuli.

AHADI UBUNGO

Akihutubia mkutano huo, Rais Magufuli aliwaahidi wananchi wa Ubungo kuwajengea barabara za mitaa, sambamba na ujenzi wa makao makuu ya Wilaya ya Ubungo, endapo akichaguliwa kwa mara ya pili.

"Madiwani chagueni eneo la kujengwa kwa makao makuu ya wilaya ili Ubungo nayo iwe na makao makuu kama ilivyo kwa wilaya zingine. Nimeteseka sana kuisaidia ubungo, ukileta mradi huu unakwama, kwa mfano ujenzi wa kituo cha mabasi Mbezi. Sasa nileteeni wabunge wa CCM na madiwani ili maendeleo yaje haraka," alisema Rais Magufuli.

**ASISITIZA AMANI**

Kadhalika, Rais Magufuli alivitaka vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi mkuu kuwa na umoja, kudumisha amani.

Pia, aliwataka Watanzania kutokubali kuiharibu amani huku akiwasisitiza kuwakataa wagombea wanaoleta viashiria vya uvunjifu wa amani.

"Watanzania tusikubali kutenganishwa kwa ajili ya uchaguzi, kuna maisha baada ya uchaguzi, wasitumie kama kichocheo cha kutugombanisha. Mnaona mataifa mengine yanavyoteseka? Maadui zetu watafurahi wakiona Tanzania inasambaratika," alisema na kuongeza:

"Niwaombe viongozi wa dini mliombee taifa hili tumalize uchaguzi salama, tuwaogope wale wanaotaka kutuchonganisha."

# ...Azuru Msikiti Mkuu Kinondoni

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS John Magufuli, ametembelea Msikiti Mkuu uliojengwa Kinondoni jijini Dar es Salaam kwa ufadhili wa Mfalme Mohammed VI wa Morocco.

Akiwa msikitini huko jana, Rais Magufuli amepokewa na Mufti wa Tanzania, Sheikh Aboubakar Zuberi, Balozi wa Morocco nchini, Abdelilah Benryane na viongozi wengine wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) ngazi ya taifa na Mkoa wa Dar es Salaam.

Ujenzi wa msikiti huo ulioanza mwaka 2018 baada ya Rais Magufuli kumwomba Mfalme Mohammed VI (aliyekuwa katika ziara ya kitaifa nchini) ajenge msikiti mkubwa kwa ajili ya waislamu wa Tanzania, umekamilika kwa asilimia 100 na sasa unasubiri kuzinduliwa rasmi.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, alibainisha kwamba, baada ya kuutembelea na kujionea ukiwa umekamilika, Rais Magufuli alielezea kufurahishwa kwake na ubora wa hali ya juu wa msikiti huo, jinsi unavyovutia na akasema ameridhishwa na kazi kubwa iliyofanywa.

"Mheshimiwa Rais Magufuli ameahidi kuandika barua ya kumwalika Mfalme Mohammed VI kuja hapa nchini kuzindua msikiti huo kama alivyoahidi na amemwomba Balozi wa Morocco nchini, Benryane kutanguliza salamu zake za shukrani kufuatia kukamilika kwa ujenzi huo," ilibainisha taarifa hiyo ya Ikulu.

Ilibainishwa zaidi katika taarifa hiyo ya Ikulu kuwa, wakiwa msikitini huko, Mufti wa Tanzania, Sheikh Zuberi, aliomba dua kwa ajili ya taifa, akimwombea Rais Magufuli, na pia shukrani kwa Mungu kwa kufanikisha ujenzi wa msikiti huo.

# TRA yasisitiza uadilifu kwa watendaji wake

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

NAIBU Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (TRA), amesema moja ya mikakati yao ni kuimarisha uadilifu katika utendaji kazi wake kwa kuunda kamati za kudhibiti uadilifu ili kuongeza mapato ya serikali.

Msafiri Mbibo alibainisha mkakati huo jijini Dodoma jana alipofungua mafunzo ya siku tatu kwa makatibu wa kamati hizo za kudhibiti uadilifu ndani ya mamlaka hiyo.

"Kama mnavyofahamu, Tanzania imeingia katika uchumi wa kati, hivyo kama tunataka kuhakikisha tunadumu katika uchumi huu wa kati au tunaenda zaidi ya tulipo, ni lazima jamii yetu iendeshe mambo yake kwa uadilifu mkubwa na taasisi kama TRA ambayo ni nyeti, ni lazima tuboreshe eneo la maadili ili kuwa na nidhamu katika suala zima la ukusanyaji kodi," alisema.

Mbibo alisema TRA ina jukumu la kukusanya kodi kwa niaba ya serikali na jukumu hilo haliwezi kutekelezwa kwa ufanisi bila kuwa na watumishi waadilifu, ikiwa ni pamoja na uwapo wa mfumo imara unaosimamia uadilifu.

"Jukumu la TRA ni kukusanya kodi ambazo zinahusisha fedha, na sisi sote tunajua kwamba fedha zina ushawishi mkubwa, lakini hata wateja wetu ambao ni walipakodi, wanaweza kuwashawishi watumishi wetu ili wasilipe kodi kulingana na uhalisia wa kodi zao na hivyo kupunguza fedha za serikali. Tukumbuke kwamba, tukiimarisha uadilifu, tutaongeza mwamko wa wananchi kulipa kodi kwa hiari." alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Mambo ya Ndani ya mamlaka hiyo, Amiram Lekey, alisema lengo la mkakati huo ni kupunguza rushwa kwa kutumia mbinu za kuzuia na kupambana na rushwa hasa katika sekta zenye vishawishi vya rushwa ikiwamo TRA.

"TRA imeunda kamati hizi katika ngazi mbalimbali kuanzia ngazi ya taasisi, mkoa, wilaya na vituo vya kodi ikiwa ni sehemu ya kutekeleza mpango mkakati wa kupambana na rushwa wa awamu ya tatu ulioanza mwaka 2017 hadi 2022," alisema.

Mafunzo hayo ya kuwajengea uwezo makatibu wa kamati hizo za kudhibiti uadilifu ndani ya mamlaka hiyo, yanashirikisha makatibu wa kamati za kudhibiti uadilifu za idara zilizopo ndani ya TRA, Chuo cha Kodi (ITA), TRA Zanzibar, vituo vya kodi na mikoa yote nchini.

Baada ya ufunguzi huo, Naibu Kamishna Mkuu huyo wa TRA, alifanya ziara ya kikazi katika ofisi za TRA zilizoko wilayani Chamwino Kongwa jijini hapa na kuwataka watumishi wa ofisi hizo kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha wanavuka malengo ya ukusanyaji kodi waliyopangiwa katika wilaya zao.

"Katika utekelezaji wa majukumu yenu, hakikisheni mnatenda jambo jema hata kama kuna changamoto mnazokumbana nazo bila kusahau kufanya kazi kwa bidii, ubunifu na heshima kwa watu wote," Mbibo aliagiza.

Naibu Kamishna Mkuu huyo anaendelea na ziara yake katika maeneo mbalimbali mkoani hapa kutembelea ofisi za TRA na kuzungumza na watumishi ili kuwapa hamasa ya kuendelea kufanya kazi kwa bidii na weledi katika majukumu yao ya kila siku.

TANGAZO


AngloGoldAshanti
GEITA GOLD MINE
TANZANIA
Mwl. Julius K. Nyerere
1922-1999
Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) wanaungana na Mh. Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wote katika kuadhimisha kumbukumbu ya miaka 21 ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwl. Julius K. Nyerere.
Katika kumuenzi Baba wa Taifa, Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) itaendelea kushirikiana na Serikali na wadau mbalimbali mkoani Geita na Tanzania kwa ujumla katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Nyerere unaendelea kuishi miongoni mwa Watanzania

OKTOBA 14 kila mwaka ni maadhimisho ya kumbukumbu ya kifo cha mwasisi wa Tanzania Baba wa Taifa Julius Nyerere.

Leo inatimia miaka 21 tangu kifo chake kilichotokea London mwaka 1999, alipokwenda kwa matibabu katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas.

Katika uongozi wake, yapo mambo mengi ambayo aliifanyia nchi hii na kubwa anakumbukwa kwa kuhimiza zaidi haki, mshikamano, umoja na amani miongoni mwa Watanzania, ili waweze kujiletea maendeleo na kuishi kwa amani.

Alifanya hivyo, kwa kuwa hayo yanabakia kuwa nyenzo msingi katika mchakato wa maendeleo ya binadamu, hivyo aliwataka Watanzania kusimama kidete kulinda umoja na amani ya taifa ambayo ni tunu ya taifa.

Wakati huu wa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu, viongozi wa serikali na wadau mbalimbali wakiwamo wanasiasa, wamekuwa wakihimiza Watanzania kuendelea kudumisha amani na mshikamano.

Kwa mantiki hiyo, hata sisi tunaona kuna haja kwa Watanzania kudumisha amani, umoja na mshikamano wa kitaifa kama njia mojawapo ya kumwenzi Baba wa Taifa aliyechangia kuifanya Tanzania kuendelea kuwa na utulivu.

Uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Jumatano Oktoba 28, usiwe ni sababu ya kuvuruga umoja na mshikamano wa kitaifa, bali amani ambayo ni chachu ya maendeleo iendelee kuwapo na Watanzania waendelee kushikamana.

Tunawakumbusha Watanzania kuwa amani ikitoweka, hata kile kidogo ambacho wamekitafuta kwa jasho, kinaweza kuondoka na nchi ikabaki kuwa ya mahangaiko huku na kule kama ambavyo inatokea kwenye baadhi ya mataifa.

Baba wa Taifa alituachia tunu kubwa ambayo ni muhimu wote tuienzi kwa vitendo ikiwa ni pamoja na kuwakomea wale ambao wataonekana kutaka kuvuruga umoja na mshikamano wa Watanzania ambao ni matokeo ya amani.

Hapa nchini, kuna makabila mengi, lakini upo umoja wa kitaifa ambao haujawahi kupata matatizo ya kabila moja kulikandamiza jingine, bali wote wanaishi kama ndugu bila kubaguana.

Nchi imefikia hapo kutokana na mchango wake, hasa kwa kukataa Watanzania kutambuana kwa makabila bali kwa Utanzania wao tu ili kila mmoja ajione yuko sawa na mwingine.

Inawezekana hata wakati anaanzisha siasa ya ujamaa, lengo lake lilikuwa kuleta makabila yote pamoja, kwa lengo kwamba waelewane, kwa kuwa ndivyo njia mojawapo inayoweza kuwaunganisha.

Katika mwendelezo huo wa kuwafanya Watanzania wawe wamoja, wanafunzi waliokuwa wakifaulu kwenda sekondari, walipelekwa mikoa mbalimbali kutoka kwao ili kuchangamana na wa mikoa mingine.

Aidha, badala ya kutumia lugha za makabila mbalimbali, mkazo wake ulikuwa kwenye Kiswahili, ambacho kinatumiwa na Watanzania wote kuanzia vijijini na mijini kama lugha ya mawasiliano.

Baba wa Taifa alidhamiria kujenga taifa, na aliwakusanya Watanzania pamoja kulingana na maeneo yao na hatimaye hadi leo ni wamoja na kinachotakiwa ni kuendelea kudumisha amani iliopo.


Hatua ya Baba wa Taifa kuanzisha taratibu hizo zote akiamini kwamba, Watanzania wakiwa pamoja, amani itakuwepo na ni rahisi kujiletea maendeleo kwa vile watu hawatakuwa na hofu.

Yapo mengi ambayo aliyafanya kwa ajili ya nchi hii, kama yanavyojulikana lakini suala la kuimarisha amani ni la muhimu, hivyo tumwenzi katika hilo, kwa kudumisha amani hata katika uchaguzi ujao.

Japo Nyerere amekufa miaka 21 iliyopita lakini hata sasa anaishi na anaendelea kuonekana katika falsafa zake za umoja na udugu, mshikamano na kuthamini utu wa mtu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Ndivyo Nyerere alivyobeba bango utetezi vyama vingi

Na Sabato Kasika

MWAKA 1992 ndiyo ambao mfumo wa vyama vingi vya siasa ulirejeshwa nchini, hatua ambayo iliwafanya baadhi ya Watanzania na hasa wanasiasa, kuanzisha 'utitiri' wa taasisi hizo.

Baadhi ya vyama vilivyoanzishwa na kupata usajili wa kudumu, vilishiriki uchaguzi mkuu wa kwanza ndani ya mfumo huo mwaka 1995, huku wanagombea wake wakishinda baadhi ya majimbo na kata.

Urejeshwaji wa mfumo huo umechangiwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ambaye mawazo yake yaliridhia vyama hivyo viwepo na sasa vinaendelea na shughuli za kisiasa.

Tanzania inapotimiza miaka 21 bila Baba wa Taifa, kuna haja ya kukumbuka mchango wake katika siasa za Tanzania, hasa urejeshwaji wa mfumo wa vyama vingi, ambao inawezekana baadhi ya Watanzania hawajui.

Wale waliozaliwa mwaka 1992, kipindi ambacho mfumo huo unarejeshwa tena wanatimiza miaka 30.

Kabla ya uchaguzi mkuu wa 1995, Rais wa wakati huo, Ali Hassan Mwinyi, aliunda Tume ya Jaji Francis Nyalali, kukusanya maoni ya kupitisha mabadiliko ya katiba ya Tanzania.

Lengo lilikuwa ni kutaka nchi kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa kutokana na mabadiliko makubwa ya duniani, lakini kwa mujibu wa tume hiyo, asilimia 20 ya Watanzania waliutaka wakati asilimia 80 ilipinga na kung'ang'ania chama kimoja.

Utaratibu huo ulioanzishwa mwaka 1965 walitaka uendelee, lakini utaratibu wa wengi wape ukawekwa pembeni na kuchukuliwa maoni ya wachache.

Hatua hiyo inatokana na maamuzi ya serikali hasa baada ya ushauri wa Baba wa Taifa ambaye aliamini kwamba, ipo siku asilimia ya waliotaka vyama vingi, itakuwa kubwa na hao ndiyo wakawa washindi.

Kuwapo kwa vyama vingi vya siasa nchini, vinavyoendelea kufanya shughuli zake ni matokeo ya uamuzi wa asilimia 20 ya waliokubali ambao uliridhiwa na serikali kwa ushauri wa Baba wa Taifa.

Baada ya kuviruhusu vyama vya siasa vilianzishwa kwa wingi ambavyo baadhi yake vilishiriki katika uchaguzi mkuu wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi, huku NCCR-Mageuzi kikiwa kinara.

Vingine ni pamoja na Tanzania Labour Party (TLP), CHADEMA, CUF na Union for Multiparty Democracy (UMD).

Wingi wa vyama hivyo ulitokana na ushauri wa Baba wa Taifa aliyetaka wajitokeze kuanzisha vyama hivyo bila kuwekewa ukomo, akiamini, vipo ambavyo vingejifia kwa kukosa uimara.

Utabiri huo unamgusa hata Augustino Mrema ambaye wakati huo alipofanya ziara za kichama, alibebwa na wanachama wa Chama cha TLP, hali iliyosababisha polisi kuingilia kati na kuwazuia kufanya hivyo.

Lakini Baba wa Taifa aliwaambia polisi wawaache wafanye hivyo na kuweka wazi kuwa, utafika wakati watachoka na kuacha na siku ilipofika walichoka na sasa hakuna anayembeba.

Miongoni mwa vyama vilivyopo katika daftari la Msajili wa Vyama vya Siasa vingi ni vile ambavyo havina nguvu, hali inayosababisha vishindwe kujiendesha kikamilifu.

Mbali na CCM, CHADEMA, ACT-Wazalendo na CUF, vilivyobaki ni kama havipo na inawezekana ni mwendelezo wa utabiri wa Baba wa Taifa kwamba Watanzania waache waanzishe vyama ila vitajifia vyenyewe.

Hili liwe somo kwa wanasiasa kuwa wanapoanzisha vyama wajitahidi kufikia malengo, ambayo ni kuongoza nchi kupitia sanduku la kura kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na Watanzania.

Hivyo wakati huu wa kumbukumbu ya miaka 21 ya kifo cha Baba wa Taifa, wanasiasa hawana budi kutafakari ushauri wake na kuufanyia kazi ili wawe na vyama vyenye nguvu kuliko kubaki wasindikizaji.

## HABARI KITAIFA

# Lissu aahidi kupandisha mishahara ya watumishi

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MGOMBEA urais (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema akichaguliwa kuwa rais katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu, atahakikisha anawapandisha madaraja na vyeo watumishi wa umma wakiwamo askari polisi wote wenye sifa.

Lissu alitoa ahadi hiyo jana alipozungumza na wananchi wa majimbo ya Kahama Mjini, Msalala na Ushetu katika Viwanja vya Lowasa mjini hapa.

Alisema serikali atakayoingoza haitanyanyasa Jeshi la Polisi kutokana na kutambua umuhimu wake katika kulinda wananchi na mali zao.

Mtaalamu huyo wa sheria alisema atawapandisha madaraja askari polisi wanakaohitaji kupandishwa vyeo na kuwaomba kusimamia haki kwenye uchaguzi mkuu, ili aliyeshinda kwa haki atangazwe kwa haki na aliyeshindwa kwa haki, atangazwe kushindwa kwa haki.

Lissu alisema asingependa kuona kunatokea upande wa kuiba kura za wagombea ngazi ya urais, ubunge na madiwani kisha kutolewa amri ya kulitaka Jeshi la Polisi kupiga watu na likaitekeleza.

Mgombea huyo pia alikumbusha namna alivyokuwa sehemu ya mapambano kwa ajili ya maslahi ya Kahama tangu mwaka 1999 hasa katika maeneo yenye wachimbaji wadogo wa madini.

Kabla ya kuanza kunadi sera zake, Lissu aliwaomba radhi wananchi wa majimbo hayo kwa kuchelewa kufika katika eneo la mkutano, akidai kuchelewa kwake kunatokana na kuanza mikutano tangu asubuhi katika Mkoa ya Singida, Tabora na Shinyanga.

Lissu aliwaomba wananchi kuhakikisha Oktoba 28 mwaka huu wanakipigia kura chama chake ili kuondoa kile alichokiita manyanyaso ya maisha na kuleta haki na heshima kwa watumishi walionyimwa haki ya kupandishwa mishahara na wachimbaji wadogo wanaoumizwa miaka yote katika uchimbaji wao.



Hata hivyo, baada ya mkutano huo, Jeshi la Polisi lilazimika kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya wafuasi wa chama hicho walipoandamana kumsindikiza Lissu hadi kwenye eneo aliloandaliwa kufikia kwa ajili ya mapumziko.

# Wanawake vijijini wapigiwa chapuo

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

MAMLAKA za Serikali za Mitaa zimetakiwa kutambua fursa, vikwazo na mafanikio ya wanawake wanaoishi vijijini ili kuwawezesha kiuchumi na kuwajengea mazingira mazuri ya kupata haki za msingi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mwanamke Anayeishi Kijijini, kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jinsia, Mboni Mgaza, alisema hatua hiyo itasaidia kupiga hatua kwa kuweka miradi endelevu ya kuwaendeleza wanawake wanaoishi vijijini.

"Lengo la maadhimisho haya ni kutambua na kuenzi mchango wa wanawake wanaoishi vijijini hususani katika nyanja za uzalishaji kwenye kilimo, ufugaji, uvuvi na ujasiriamali ili kuhakikisha usalama wa chakula wa kaya, hivyo kuchangia uchumi wa Taifa," alisema Mgaza.

Alisema kuwa siku hiyo inalenga kuwaunganisha wanawake na wadau katika mtandao wa kibiashara ili kuhakikisha wanafaidika na mfumo wa kifedha wa kidijitali.

Pia alisema kuwaelimisha wanawake jinsi ya kupata teknolojia rahisi na sahihi za uzalishaji ili kuweza kumudu ushindani wa biashara katika masoko ya ndani na nje ya Tanzania.

"Asilimia 65 ya wanawake wako katika sekta ya kilimo ambayo inaonyesha kuwa wanachangia kwa kiasi kikubwa uzalishaji mazao ya kilimo na serikali imechukua hatua mbalimbali kuboresha miundombinu vijijini ikiwa ni hatua kubwa kuwainua wananchi hususani wanawake," alisema.

Maadhimisho ya Siku ya Mwanamke Anayeishi Kijijini huadhimishwa kila Oktoba 15 na mwaka huu yatafanyika katika kijiji cha Kazole, mkoani Pwani huku kila mkoa na halmashauri zikiadhimisha siku hiyo kwenye maeneo husika.

Kaulimbiu ya siku hiyo ni "Mwanamke Anayeishi Kijijini ni Msingi na Ustawi wa Maendeleo ya Nchi".




# Askofu Katoliki ahimiza elimu ya dini kwa watoto

**Na Jumbe Ismailly, MANYONI**

ASKOFU wa Jimbo Katoliki Singida, Mhashamu Edward Mapunda, amewaagiza watawa wa jimbo hilo kuongeza jitihada za kuwekeza kwa watoto kwa kuwafundisha elimu ya dini, ili wao watakapostaafu wawepo watakaochukua nafasi zao.

Baba Askofu Mapunda alitoa wito huo kwenye Jubilee ya miaka 25 ya watawa sita iliyofanyika katika mji mdogo wa Mitundu, Tarafa ya Itigi wilayani Manyoni.

Alisisitiza kwamba bila kuwafundisha watoto elimu ya dini, kuna uwezekano mkubwa wa kutopatikana kwa watawa wa siku za baadaye, jambo ambalo linaweza kuhatarisha amani, utulivu na hata upendo miongoni mwao.

Alisema ni jukumu la watawa hao kuwakomboa watu hao kimwili kutokana na maarifa waliyonayo na kuwataka wajitahidi kubadilisha fikra za watu, kubadilisha mioyo ya watu ili watu wasiendelee kufanya kazi kwa mazoea kwa sababu wao wana elimu na maarifa mengi.

"Kwa mfano tunaona wanafuga na wana miradi ya nyuki na wanataka eneo lao la ufugaji wa nyuki liwe mfano wa kuigwa na majirani wanaolizunguka eneo a masista," alifafanua Askofu Mapunda.

"Wito wa mapadri na masista ni kufundisha dini, hivyo ni wajibu wao kuwekeza elimu ya dini kwa watoto ili kutekeleza wito unavyowataka," alisisitiza.

# Wahukumiwa kulipa faini ya mil. 16/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imewahukumu wafanyabiashara wanne wakiwamo raia wawili wa Kenya kulipa fidia ya Sh. milioni 16 kwa kosa la kuisababishia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) hasara ya Sh. milioni 16.6.

Washtakiwa hao ni Beth Ngunyi (43) mfanyabiashara na Mkazi wa Kasaram Nairobi, Frolence Dirango (34) mfanyakazi wa Kampuni ya Betlee kama Ofisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Alven Swai (26) mkazi wa Mbezi Beach na Godluck Macha (28) mfanyabiashara na mkazi wa Mbezi Beach, wamehukumiwa kulipa fidia hiyo baada ya kuingia makubaliano na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi Yusto Luboroga.

Hakimu alisema Ngunyi na Wanjira wametakiwa pia kulipa faini ya Sh. 500,000 kila mmoja kwa kosa la kuishi nchini bila vibali maalum vinavyotambulika kisheria. Aidha, mahakama hiyo pia imetaifisha vifaa vya kielektroniki ikiwamo kompyuta mbili za mpakato, mashine mbili za kuunganisha intaneti na laini za simu zaidi ya hamsini ambazo washtakiwa hao wanadaiwa kuvitumia kutenda uhalifu wa kimtandao.

Hata hivyo, washtakiwa hao wamefanikiwa kulipa faini hiyo baada ya kufikia makubaliano na DPP kukiri makosa yao.

Awali ilidaiwa Julai 13, mwaka huu eneo la Tarakea wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro, Ngunyi na Dirangu waliingiza vifaa vya kielektroniki nchini pasipo kuwa na leseni ya TCRA.

Mushi alidai Julai 20, mwaka huu, maeneo ya Kibona Lodge Mbezi Beach jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao walisimika vifaa vya mawasiliano bila kuwa na leseni kutoka TCRA.

Katika mashtaka ya nne, inadaiwa kati ya Julai 20 na 26, mwaka huu maeneo ya Kibona Lodge Mbezi Beach, kinyume cha sheria walifanyia marekebisho ya vifaa hivyo vya kielektroniki.

Pia inadaiwa kinyume cha sheria washtakiwa hao waliendesha mitambo ya mawasiliano bila kuwa na leseni.

Mushi alidai kinyume cha sheria washtakiwa hao walitumia vifaa vya mawasiliano vilivyounganishwa na vifaa vingine vya mawasiliano kwa nia ya kupokea na kusambaza mawasiliano bila kupata uthibitisho wa TCRA.

Washtakiwa hao wanadaiwa walikwepa kufanya malipo ambayo yalipaswa kufanyika kwa kuruhusu mawasiliano nje ya nchi kutokana na kutumia kifaa hicho cha mawasiliano bila kuwa na leseni.

Katika shtaka la tisa, inadaiwa Julai 13, mwaka huu maeneo ya Kibona Lodge, Mbezi Beach, Ngunyi na Dirangu wanadaiwa kuwapo nchini bila kuwa na kibali.

Macha anadaiwa Julai 15, mwaka huu kinyume cha sheria aliwahifadhi Ngunyi na Dirangu kuishi nchini wakati wakijua hawana kibali.

Katika mashtaka ya 11, inadaiwa kati ya Julai 20 na 26, mwaka huu maeneo ya Kibona Lodge Mbezi Beach jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao waliisababishia TCRA hasara ya Sh. 16,634,400.






## Wakulima, w'biashara kupata mikopo nafuu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA, wafanyabiashara wakubwa na wadogo wameahidiwa kusaidiwa katika kukuza shughuli zao za kiuchumi.

Makundi hayo yamehakikishiwa na Benki ya NMB kuwezeshwa kwa kupatiwa mikopo yenye riba nafuu ambayo ni rafiki kwa shughuli zao, ili waweze kukuza uchumi wao binafsi na taifa kwa ujumla.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Idara ya Biashara wa benki hiyo, Alex Mgeni, wakati akizungumza na makundi ya wajasiriamali, wakulima na wafanyabiashara wa mikoa ya Njombe, Iringa na Mbeya kwenye kikao cha tathmini ya mwenendo wa benki hiyo kilichofanyika Mjini Makambako.

Mgeni alisema idara hiyo imekuwa ikisikiliza mahitaji ya wateja wake ambao waliowengi ni wakulima, wafanyabiashara wadogo na wakubwa, ambapo katika suala la mikopo wengi wamekuwa wakishauri kutolewa kwa mikopo yenye unafuu kwao.

Alisema kupitia maoni yao mbalimbali, NMB imeendelea kuboresha eneo hilo la mikopo, ikizingatia kuwa makundi hayo bila ya kusaidiwa kulingana na mazingira yao ya ufanyaji shughuli zao kwa ufasaha uchumi wa nchi hauwezi kukua.

Meneja Mwandamizi Idara ya Kilimo, Wogofya Mfalamagoha, alisema kuwa katika kuhakikisha Watanzania wanakopesheka zaidi, wapo katika hatua za mwisho kuanza kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika shughuli za urasimishaji ardhi.

Aidha, alisema benki hiyo inatoa mikopo ya vifaa mbalimbali kwa ajili ya shughuli za kilimo ikiwamo trekta na mashine za kuchakatia mbao kwa masharti nafuu na inalipwa kwa miaka mitatu na kila mwaka mkulima analipa mara moja baada ya mavuno.

Katika hatua nyingine benki hiyo ilikutana na wafanyabiashara wa Mkoa wa Mbeya katika kongamano lililofanyika Mjini Mbeya ambalo mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila.

Chalamila aliwataka wafanyabiashara mkoa huo kuwa wabunifu katika biashara na kulipa mikopo kwa wakati ili kukuza mitaji.

Aidha, Chalamila alisema asilimia kubwa ya wafanyabiashara nchini wakiwamo wa mkoa wa Mbeya hawana desturi ya kutunza kumbukumbu na hivyo kushindwa kukopesheka na benki kubwa.

Kabla ya kongamano hilo benki hiyo ilifanya kikao kilichowahusisha wafanyabiashara na wateja (Business Club) ambapo benki hiyo ilibainisha namna ilivyoweza kukabiliana na ugonjwa hatari wa COVID-19 kusaidia changamoto za kibiashara kwa wafanyabiashara kwa kurekebisha mikopo kwa kuwapa nafuu ya urejeshaji wa mikopo.

Meneja Mwandamizi Kitengo cha Biashara, Machaga Changarawe, alisema, athari iliyotokana na ugonjwa huo iliwakumba wateja wake, benki ilitumia fursa hiyo kukaa nao na kutoa muda wa kulipa mikopo na hata kusimamisha baadhi ya marejesho kwa wakopaji wake.

## Mongella: Ulinzi mipaka kichocheo cha maendeleo

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, amesema kulinda mipaka ya nchi na kufuata sheria ndio msingi wa wananchi kujiletea maendeleo.

Aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na maofisa wakuu kutoka Chuo cha Ukamanda na Unadhimu kilichopo eneo la Duluti, Wilaya ya Arumeru Mkoa wa Arusha.

Alisema shughuli mbalimbali za maendeleo zinazofanywa na wananchi zimeufanya Mkoa wa Mwanza kukua kwa kasi na kuchangia asilimia 32.4 la pato la taifa.

Aliongeza kuwa wana fursa mbalimbali za kiuchumi, huku wao wakiwa wamewekeza katika sekta ya uuvi, kilimo, biashara na viwanda pia usafirishaji wa samaki kwenda Ulaya ni fursa kubwa inayochochea kukuza uchumi wa wakazi na taifa.

Brigedia Jenerali Sylvester Ghuliku, Mkuu wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu, Duluti Arusha, alisema wanatoa mafunzo kuanzia cheo cha meja na kuendelea ili kuwajengea uwezo kukabiliana na matatizo mbalimbali ya utendaji, na kuwa chuo kinachukua wanafunzi kutoka ndani na nje ya nchi.

Alisema katika awamu hii wana wanafunzi 65 ambao wapo katika makundi mawili, moja likiwa Dar es Salaam na lingine Mwanza, lengo likiwa baada ya mafunzo ya darasani wanatoka nje kwenye maeneo ya wananchi kwa ajili ya kufanya utafiti na kuona vitu vinavyoendelea katika shughuli za uraiani.

## Upatikanaji maji Kagera waongezeka

**Na Mwandishi Wetu**

MKOA wa Kagera umekamilisha jumla ya miradi ya maji 73 yenye thamani ya Sh. 62,516,688,102.

Hali hiyo imeongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi kutoka asilimia 42 iliyokuwapo mwaka 2015 katika miji hadi kufika asilimia 65 iliyopo sasa na kwa vijijini kutoka asilimia 53 hadi asilimia 67.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mkoa wa Kagera, Mhandisi Warioba Sanya, amesema hayo na kuongeza lengo ni kufika zaidi ya asilimia 85 kwa vijijini.

Amesema kwa miji ongezeko hilo ni kwa miji ya wilaya na mkoa ambapo inatarajiwa kiwango cha upatikanaji maji kuongezeka kwa sababu ya uwekezaji katika miradi inayoendelea.

Alitolea mfano wa Manispaa ya Bukoba ambapo kwa sasa upatikanaji maji ni asilimia 90 ambayo itapanda hadi kufikia asilimia 95 ifikapo Juni 2021 baada ya mtandao wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bukoba (BUWASA) kuongezwa katika maeneo ya pembezoni.

Alifafanua kuwa kuna ujenzi wa miradi mikubwa ya maji mjini inayohusisha ujenzi wa miradi ya maji katika mji wa Kayango wilayani Karagwe, Mji wa Kyaka-Bunazi wilayani Misenyi, Mjini Kemondo hadi Maruku wilayani Bukoba, Mji wa Biharamulo na ujenzi wa mradi wa mifumo ya maji taka Mjini Bukoba.

# Mwekezaji ajenga shule, aikabidhi kwa serikali

**Na Richard Makore,** MWANZA

SERIKALI imesema ipo tayari kupokea wawekezaji wa sekta mbalimbali na kuwasikiliza ili kutatua changamoto wanazokutana nazo kwa lengo la kuwasaidia waweze kuwekeza na kufanya biashara katika mazingira mazuri.

**Kuna mpango wa baadaye wa kununua meli nyingine kubwa ya kisasa ambayo inavua kwa kutumia vyavu, ingawa gharama yake ni kubwa.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Nchini (TIC), Dk. Maduhu Kazi, aliyasema hayo jana wakati akipokea shule ya sekondari na chuo cha ufundi vyenye thamani ya Sh. milioni 330 vilivyojengwa na kiwanda cha kuchambua pamba cha Alliance Ginnery.

Dk. Kazi alisema serikali inahitaji wawekezaji, lakini inataka wawe wanaisaidia jamii inayowazunguka na kusogeza mbele maendeleo yao.

Alisema TIC muda wote milango ipo wazi ili kuhakikisha inakuwa na taarifa za kila mwekezaji na kujua kama anakabiliwa na changamoto yoyote na kuitatua haraka.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kwa sasa wanatumia teknolojia ya kisasa katika kufanya mawasiliano na wawekezaji pamoja na kutumia ofisi za kanda ili kuhakikisha kila mfanyabiashara anawekeza katika mazingira yasiyokuwa na usumbufu ama urasimu.

"Hiki kiwanda kimezingatia maagizo ya serikali ya awamu ya tano, tunahitaji wawekezaji kama hawa ambao wanaisaidia jamii inayowazunguka siyo wawekezaji wanaokwenda kuchimba mashimo mawili ya choo halafu wanasema wameisaidia jamii," alisema Dk. Kazi.

Aliwataka watu wanaotaka kuwekeza katika Kanda ya Ziwa kutumia ofisi za TIC zilizopo mkoani Mwanza na kwamba bado kuna fursa nyingi katika eneo hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kalli, alisema tatizo la watoto kutembea umbali mrefu kwenda shule sasa limekwisha.

Aidha, aliomba TIC kuendelea kutafuta na kupokea wawekezaji ambao wanaisaidia jamii inayowazunguka na kwamba serikali ngazi ya wilaya ipo tayari kushirikiana nao.

Shule hiyo iliyojengwa katika kijiji cha Bugatu wilayani Magu, imegharimu Sh. milioni 150, ina madarasa, ofisi za walimu pamoja na vyoo vya wasichana na wavulana.

Akizungumza wakati wa kupokea chuo cha ufundi kilichojengwa na kiwanda hicho katika kijiji cha Kasori wilayani Busega mkoani Simiyu, Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka, aliagiza wasichana wote waliomaliza darasa la saba kuanza kusajiliwa ili waanze kupata mafunzo.

Alisema serikali inaunga mkono wawekeza na kwamba TIC imekuwa ikifanya juhudi ili kuhakikisha mazingira ya uwekezaji yanakuwa rafiki kwa kila mfanyabiashara.

Meneja wa Kiwanda cha Alliance Ginnery, ambacho kimejenga shule pamoja na chuo hicho, Boaz Ogola, alisema wametoa msaada huo baada ya kuona watoto wa eneo hilo wakitembea umbali mrefu kwenda shule.

Alisema shule ya sekondari imegharimu kiasi cha Sh. miloni 150 na chuo cha ufundi Sh. milioni 180 hadi kukamilika kwake.



Rais mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete akijadiliana jambo na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Vodacom Tanzania Plc, Margaret Ikongo (katikati) na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Hisham Hendi, wakati wa hafla ya kuchangia fedha kwa ajili ya watoto wenye usonji, iliyoandaliwa na Lukiza Autism Foundation, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bashe azindua kiwanda cha pamba

**Na Mwandishi Wetu,** CHATO

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amezidua Kiwanda cha Pamba cha Chato (CCU) na kuielezea hatua kama mpango kabambe wa serikali wa kujenga sekta ya kilimo inayojitegemea sambamba na uhakika wa upatikanaji wa malighafi.

Akizungumza baada ya kukizindua mwishoni mwa wiki, Waziri Bashe alisema kufufuliwa kwa kiwanda hicho mwanzo mzuri kwa wakulima pamba kuongoza uzalishaji na kuinua vipato vyao.

"Mradi wa kufufua kiwanda hiki umegharimu jumla ya Sh. 6,714,804,447 kutoka katika benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), lengo likiwa kuimarisha sekta ya kilimo ili kuwanufaisha wakulima wa pamba," alisema Bashe.

Alisema kufufuliwa kwa kiwanda hicho ambacho kilisimama kufanya uzalishaji kwa miaka kadhaa kutawafanya wakulima wilayani Chato na maeneo mengine ya jirani kuongeza uzalishaji, hivyo kuleta unafuu wa maisha kwa wakulima.

"Serikali imedhamiria kuifanya sekta ya kilimo inajitegemee kwa kuwa mbali ya kutoa ajira kwa Watanzania walio wengi, pia imekuwa na mchango wa asilimia 25 katika pato la Taifa," alisema.

Aidha, waziri Bashe aliipongeza benki hiyo kwa jitihada zake za kuwaletea wakulima maendeleo kwa kuwapa mikopo yenye masharti nafuu jambo ambalo linaongeza tija katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema kuzinduliwa kwa kiwanda hicho kutaongeza thamani ya zao la pamba ambayo ilishuka tangu msimu wa 2013/14.

"Tunaamini hatua tunazochukua kwa mazao ya kimkakati ikiwamo zao la pamba iyasaidie katika kuongeza thamani yake na hivyo kuwa na bei ambayo itamfanya mkulima anufaike zaidi na kuchangia ukuaji wa pato la Taifa," alisema.

Alisema bei ya msimu huu imekuwa nzuri ukilinganisha na misimu kadhaa ya hapo awali, na kwamba wataendelea kuimarisha upatikanaji wa soko zuri na lenye faida kwa mkulima.

Kiwanda hicho kitanufaisha Vyama vya Ushirika wa kilimo na Masoko (AMCOS) 52 vyenye jumla ya wakulima 7,000 kutoka Chato, Biharamulo na Muleba.

## HABARI KITAIFA

# Watumishi wa Bandari kortini kwa mashtaka 26

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WATU watatu waliokuwa watumishi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) mkoani Kigoma na mfanyabiashara mmoja wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoa huo, wakikabiliwa na makosa 26.

Makosa hayo yanadaiwa kutendeka kuanzia mwaka 2015 hadi Januari 2020 na kuisababishia mamlaka hiyo hasara ya zaidi ya Sh. milioni 600.

Kesi namba 05 inayowakabili Eliya Stephano Ntinyako Mkurugenzi wa Kampuni ya Ntinyako Company Limited, Morris Mchindiuza; aliyekuwa meneja wa bandari ya Kigoma, Herman Ndibondo; aliyekuwa ofisa uhasibu, Lusubilo Anoisye na aliyekuwa ofisa rasilimali watu.

**Washtakiwa wataendelea kuwa rumande kutokana na makosa yanayowakabili kutokuwa na dhamana.**

Wakisoma mashtaka yanayowakabili kwa awamu, mawakili upande wa serikali, Riziki Matitu, Bonifance Kamwesige na Dismas Muganyizi mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Kigoma aliyesikiliza kesi hiyo, walidai washtakiwa hao kwa nyakati tofauti walishirikiana kutenda makosa hayo.

Makosa yanayowakabiri ni kuongoza genge la uhalifu, ufujaji na ubadhirifu, uhujumu uchumi, utakatishaji fedha na kuisababishia mamlaka hiyo hasara.

Washtakiwa hao wanaungana na washtakiwa watano ambao walifikishwa kwenye mahakama hiyo mwishoni mwa Agosti kwa makosa 54, ambapo washtakiwa wawili wakiwa wapya na wawili wakiwa kwenye kesi nyingine ambayo inaendelea mahakamani hapo.

Washtakiwa wataendelea kuwa rumande kutokana na makosa yanayowakabili kutokuwa na dhamana, huku kesi hiyo ikipangwa kutajwa tena Oktoba 26, 2020.



Ofisa Uvuvi Mwandamizi Nelson Mbawala (kushoto), akitoa maelezo ya jinsi ufugaji bora wa samaki unavyofanyika, kwenye mabanda ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, katika maonyesho ya maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani kitaifa, yanayoendelea kwenye viwanja vya Mjimwema mkoani Njombe. **MPIGAPICHA WETU**

# Prof. Mkumbo akosoa vyama vya upinzani

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA ubunge Jimbo la Ubungo, mkoani Dar es Salaam, kupitia CCM, Prof. Kitila Mkumbo, amesema baadhi ya vyama vya siasa vinakabiliwa na ukata kipindi hiki kwa sababu vinalifanya suala la uchaguzi mkuu kama ni tukio badala ya kufanya maandalizi ya muda mrefu kwa kuwekeza kwenye rasilimali.



Prof. Mkumbo alisema hayo juzi wakati akihojiwa kwenye kipindi cha Dakika 45 mwishoni mwa wiki kinachorushwa na runinga ya ITV.

"Chama kimesimamisha mgombea urais na wabunge halafu hakifanyi kampeni, hakuna sababu nyingine zaidi ya ukata, hawana rasilimali na hii sababu kubwa ni kwamba vyama vya upinzani vinafanya uchaguzi kama ni tukio havifanyi maandalizi mapema," alisema.

Alisema tofauti ya CCM na vyama vingine ni kwamba huwa inafanya maandalizi ya muda mrefu miaka mitano kabla ambapo alitolea mfano uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka 2025 maandalizi yake yataanza baada ya uchaguzi huu kuisha.

Kuhusu vyama vya upinzani kuikosoa CCM na CCM nayo kuvikosoa, Prof. Mkumbo alisema hiyo ndio siasa cha msingi ukosoaji uzingatie kwenye masuala ya utawala na eneo la utendaji.

"Mfano mtu anakuja na hoja kwamba tunataka mamlaka kamili huko Zanzibar, tafsiri yake ni kwamba anataka kuvunja muungano, ambao CCM ni moja ya alama yake kubwa au mtu anakuja na sera ya kugawa nchi, anaonyesha utawala wa majimbo, huyu hatufai, anataka kuivunja nchi," alisema.

Alisema viongozi wanaozungumza mambo kama hayo hawawezi kuachwa hivi hivi ni lazima wakosolewe, mfano suala la majimbo huku ni kutaka kuturudisha utawala wa majimbo ambao Mwalimu Julius Nyerere rais wa kwanza aliuvunja miaka mingi iliyopita.

## DUWASA yapewa bil. 1/- kutatua kero ya maji

**Na Happiness Shayo,** DODOMA

SERIKALI kupitia Wizara ya Maji imeipatia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), shilingi bilioni moja ili kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo yenye changamoto ya huduma hiyo jijini humo.

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji, Anthony Sanga, alisema hayo alipotembelea kisima kimojawapo kati ya vinavyochimbwa katika eneo la Ihumwa.

"Hili linafanyika kutokana na ongezeko la mahitaji ya huduma ya maji katika maeneo mbalimbaji ya Jiji la Dodoma hasa maeneo ya pembezoni," alisema Sanga.

Amefafanua kuwa, kuhamia kwa serikali jijini Dodoma ni fursa kwa taasisi za maji za jiji hilo kutatua changamoto za huduma hiyo wanazozipata wananchi.

Mhandisi Sanga ameongeza kuwa serikali ina mipango ya muda mfupi, ya kati na mrefu ya kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma ya maji.

"Mipango ya muda mfupi ni kama ujenzi wa visima vya dharura katika eneo la Ihumwa na mipango ya muda wa kati ni ujenzi wa bwawa la Farkwa na muda mrefu ni kutoa maji kutoka Ziwa Victoria," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi David Pallangyo, alisema ujenzi wa kisima hicho eneo la Ihumwa ni kimojawapo vitakavyoweza kuzalisha maji na kuyatoa kuyapeleka hadi mjini ili kupunguza tatizo eneo la mjini.

## Mradi kudhibiti mimba za utotoni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wanaosoma Shule ya Sekondari na Msingi Mwantini wilayani Shinyanga, wamejengewa uwezo wa kuanzisha mradi wa ufugaji kuku, kwa ajili ya kupata fedha ambazo zitawasaidia kutimiza mahitaji yao ya shule, ili kutojiingiza kwenye vishawishi vya mahusiano na kutimiza ndoto zao.

Imebainishwa baadhi ya wanafunzi wa kike wamekuwa wakijiingiza kwenye mahusiano ya kimapenzi baada ya kukosa mahitaji yao muhimu ya shule, na kujikuta wakiambulia ujauzito na kuacha masomo kisha wengine kuolewa na kuzima ndoto zao.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkurugenzi wa Shirika la Invest in Child and Their Society (ICS) la mkoani Shinyanga, Kundely Sokoine, kwenye ziara ya viongozi kutoka wizara tano, namna wanavyotekeleza miradi ya kupambana kutokomeza matukio ya ukatili wa kijinsia ndani ya jamii, likiwamo tatizo la mimba na ndoa za utotoni.

Alisema mbali na utoaji wa elimu kwa wanafunzi juu ya kujitambua, pia wanawajengea uwezo jinsi ya kufanya shughuli mbalimbali za kiujasiriamali bila ya kuathiri masomo yao, ili wapate fedha za kutimiza mahitaji yao ya shule, na kutojiingiza kwenye mahusiano ya kimapenzi ambayo yamekuwa yakizima ndoto zao.

## Nyerere; kinara kodi kwa maendeleo

Ukurasa 12





Ukurasa 13

## Kuuishi wosia huu wa Baba wa Taifa ndiko kuipenda Tanzania

siasa

JUMATANO OKTOBA 14, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

UCHAMBUZI

# Nyerere kinara nishati

- Baba mabwawa Nyumba ya Mungu, Mtera, Hale
- Msomi ashauri kumwenzi kwa vinu vya nyuklia

**Na Gaudensia Mngumi**

KATIKA mambo ambayo Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, aliyatamani ni pamoja na kuona Tanzania yenye umeme. Alitaka kuliona taifa liking'aa kuanzia Mtwara mpaka Mara, Tanga hadi Tabora tena Kigoma hadi Kilimanjaro, kukiwaka umeme bila kujali ni mjini au kijijini.

Ndiyo maana awamu ya kwanza inaheshimika kwa kujenga mabwawa mengi ya kufua umeme wa maji mfano Nyumba ya Mungu, Kidatu , Mtera, Hale na Pangani ni jitihada ambazo zilizalisha megawati za umeme takribani 320 kwa miaka hiyo.

Baba wa Taifa aliaga dunia Oktoba 14, 1999 katika hospitali ya Mtakatifu Thomas Uingereza.

Hatua hiyo ya Mwalimu kuitaka Tanzania na Zanzibar zenye mwanga ilifanikisha ujenzi wa waya wa umeme wa baharini uliopeleka nishati hiyo Unguja kwa kupitisha waya baharini.

Sera ya Nishati ya Taifa ya mwaka 2013 inataja umeme wa maji kuwa ni kipaumbele cha taifa, aidha inaipa nishati ya nyuklia kipaumbele cha pili.

Hivyo, katika kumuenzi Nyerere aliyewekeza kwa nguvu uzalishaji wa nishati nchini, taifa linaitazamaje sera ya nishati kwa kufikiria kuanza uzalishaji wa umeme wa nyuklia ambao ni endelevu na wenye tija zaidi hasa kwa kipindi hiki cha mabadiliko ya taibianchi?

Ni swali Nipashe inalomuuliza mbobezi wa nishati, Dk. Kamugisha Byabato wa Kitivo cha Uhandisi cha Chuo Kikuu cha St. Augustine Tanzania mkoani Mwanza.

Dokta Byabato anajibu kwa kumpongeza Rais John Magufuli, kwa kufanya maajabu kwa kuweka kwenye ujenzi wa bwawa la umeme wa maji a Mwalimu Nyerere ambacho ni kielelezo cha kutekeleza Sera ya Taifa ya Nishati.



"Nampongeza sana Rais John Magufuli, ameonyesha njia ya kuwa na uchumi wa viwanda ambao kuwa na umeme wa uhakika ni moja ya vigezo vinavyohitajika. Kujenga bwawa la Nyerere la kufua umeme wa kilowati 2,100 ni jitihada kubwa zinazoendana na sera yetu ya nishati,"anasema.

Anashauri kuwa pamoja na kazi nzuri awamu zijazo na wataalamu wakiwamo wasomi vyuo vikuu, Tume ya Sayansi na Teknolojia, Tume ya Nguvu za Atomiki, zianze kufikiria mchakato wa kujenga vinu vya nyuklia, anasema mhandisi huyo.

Anasifu hatua za serikali za kuongeza umeme nchini ikiwamo miradi ya gesi, makaa ya mawe, jua, upepo na sasa bwawa la Mwalimu Nyerere au Stiegler's gorge lakini... "Ni muhimu tuanze mchakato wa umeme wa nyuklia. Hata kama nchi zilizoendelea hazitaki twende huko tuamke. Wanakataa kwa sababu wanajua hili ni eneo lao la kujidai" anasema Dk. Byabato.

Anakumbusha kuwa urani na platiniam zinachukuliwa Afrika kwenda kuzalisha umeme Ulaya akitoa mfano wa Niger, inayouza urani yake ng'ambo lakini nchi hiyo iko gizani. Mataifa tajiri hayawezi kukubali Afrika ifikie huko.

"Nampongeza Rais John Magufuli kwa kuona umuhimu wa umeme na kufanya jitihada hizo. Niko tayari leo akiniita nimshauri kuhusu uwekezaji huo na kutoa mchango wangu kwa taifa langu. Ndiyo maana nasema tunahitaji kuwa na umeme wa nyuklia tuanze kufikiria mpingo yake kuanzia sasa." Anasema .

Anaongeza kuwa taifa linaelekea kwenye uchumi wa viwanda ambao ni mkubwa ni vyema kufikiria uwekezaji huo wa vinu vya nyuklia ili kuwa na umeme wa kutosha.

Anakumbusha kuwa taifa lina urani ya kutosha lakini kuna siasa za kukataza kuitumia kwa hofu kuwa ina athari jambo ambalo si kweli wakati wote.

"Madini hayo yana mnururisho (reactive materials) yana uwezo mkubwa wa kuzalisha umeme mwingi na kwa miaka mingi ndiyo maana Ulaya, Ufaransa, Marekani, Korea na Japan hawafungi vinu vya zamani."

Wanachofanya sasa ni kuviboresha kupunguza athari lakini kupata umeme zaidi na kwa tija kubwa kwa vile ndiko kuliko na umeme mwingi na wa uhakika.

Dokta Byabato anasema baadhi ya mataifa ya Afrika Mashariki ya Kenya na Rwanda yameanza mchakato wa nishati ya nyuklia na na kushauri Tanzania ianze kujipanga kwenye uzalishaji huo.

### KITISHO TABIANCHI

Dokta Byabato anasema licha ya Tanzania kuwa na kipaumbele cha nishati ya maji kitisho cha mabadiliko ya tabianchi ni kikubwa na ukame ni kikwazo kikuu kwa umeme huo.

Anakumbusha kuwa nyuklia haiathiriwi na tabia nchi inaweza kuishi hata miaka 80 ni eneo la kufikiria na kuanzia sasa taifa lifikirie uwekezaji wa kuzalisha umeme wa nyuklia wakati huu tunapomuenzi Nyerere na mwasisi wa miradi mikubwa ya umeme nchini.

Tanzania ina madini ya urani yanayoweza kuzalisha umeme kwenye migodi ya Namtumbo, Ziwa Mkuju, Bahi, Galapo, Minjingu, Mbulu, Simanjiro, Lake Natron, Manyoni, Songea, Tunduru, Madaba na Nachingwea na uwekezaji unaendelea Ziwa Mkuju .

### NYUKLIA AFRIKA

Mataifa 10 ya Afrika yamo kwenye mpango wa kujenga umeme wa nyuklia na tayari, Ufaransa, Russia na China zimeonyesha nia ya kuyasaidia kufikia azma hiyo kwa upande wa teknolojia.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Nishati ya Atomiki (IAEA) , linasema ifikapo mwaka 2025 nchi tano za Afrika zitakuwa na umeme huo nazo ni Algeria, Morocco, Tunisia, Misri, Ghana, Kenya, Uganda, Zambia, Niger, Nigeria na Sudan.

"Nishati ni suala muhimu kwa Afrika kutokana na ongezeko la watu , kujenga uchumu, kutoa huduma, miundombinu na viwanda umeme kwa kila nchi hivyo mahitaji ya umeme ni makubwa na teknolojia ya nyuklia inaweza kuwa jibu."

Wataalamu wa nishati ya atomiki wanaeleza kuwa Afrika inahitaji kinu cha nyuklia chenye uwezo wa kuzalisha gigawati 160 ifikapo mwaka 2050 na kuanzia hapo idadi ya watu takribai bilioni mbili hawatakuwa na shida ya umeme kwani kwa sasa idadi ya watu ni bilioni 1.3 na wengi wanashida ya umeme hasa Kusini ya jangwa la Sahara.

Afrika inakadiriwa kuwa na zaidi ya asilimia 20 ya madini ya urani duniani na karibu mataifa 34 ya Afrika yana kiwango kibwa cha madini hayo zikiwamo Afrika Kusini, Malawi, Namibia, Niger na Tanzania.

# Nyerere; kinara kodi kwa maendeleo

## • 'Control number' inavyotimiza azma yake

**Na Mwandishi Wetu**

MWALIMU Julius Nyerere, aliyezaliwa Aprili 13, 1922 mkoani Mara katika Kijiji cha Mwitongo, anatimiza miaka 21 tangu alipofariki dunia baada ya kulitumikia taifa na kulifanyia mambo makubwa, kuanzia siku Tanzania ilipopata uhuru.

Ni miaka 21 bila Nyerere, ambayo taifa imepitia mambo mengi hasa yanayolenga kuboresha maisha ya Watanzania na kuifikisha Tanzania kule ambako Nyerere alitamaini kuipeleka, ambako si kwingine bali ni kwenye kilele cha kujitegemea kama taifa huru na kuwa na maendeleo endelevu.

Baba wa Taifa aliaga dunia Oktoba 14, 1999 katika hospitali ya Mtakatifu Thomas Uingereza.

Baada ya kung'atuka aliliacha taifa kwenye uelekeo mwingine wa kiuchumi ambao sekta binafsi na wafanyabiashara walianza kuwa sehemu ya uwekezaji wa kichumi badala ya ilivyokuwa wakati wake ambao mzalishaji na mfanyabiashara mkuu alikuwa ni mashirika na kampuni za umma.

Hivyo, suala la kulipa kodi ya moja kwa moja au kukusanya mapato kutoka kwenye mashirika hayo halikuwepo, licha ya kwamba yalitarajiwa kuipa serikali gawiwo.

Hata hivyo, baada ya kung'atuka wafanyabiashara na sekta binafsi iliibuka na kuwa mwanzo mzuri wa serikali kukusanya kodi kutoka sekta hiyo na Mwalimu Nyerere alisisitiza umuhimu wa kodi, tozo na ushuru kupata fedha za kuendesha majukumu ya serikali.

Baada ya miaka 21 ya kuondokewa na mwasisi wake, taifa limechukua juhudi zaidi kuendeleza azma ya kujitegemea kwa kukusanya mapato ya ndani ili kujiimarisha kiuchumi na kuwa taifa lisilombaomba.

Zama hizi ni mabadiliko na mapato ya serikali yanakusanywa kwa njia ya 'kontrol namba'.

'Kontroli namba' ni mfumo wa kufanya malipo ya serikali na taasisi zake yanayofanywa kwa namba maalumu anayopewa mlipaji au mteja, anasema Samuel Monyo, mtaalamu wa fedha na biashara wa kijitegemea anayefanyakazi mkoani Arusha.

"Lengo ni kuwa na mfumo madhubuti wa malipo , kuepusha udanganyifu, kulipa fedha zinazohitajika bila kupunjwa au kupunguzia serikali pesa zake na pia kuona kuwa inalipwa kwa wakati ," anaongeza.

Anafafanua zaidi kuwa Watanzania wengi wamekutana na 'kontroli namba' kwenye kulipia gharama za kuwekewa umeme na TANESCO, kulipia huduma za afya kwenye mfuko wa NHIF na wafanyabiashara kulipia kodi TRA.

Monyo anaiambia Nipashe kuwa kwenye malipo ya mara kwa mara yanayofanywa na ofisi kama akiba za wafanyakazi zinazoingizwa kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kampuni au shirika linakuwa na ' kontroli namba' ya kudumu.

Anasema mteja anakwenda kwenye taasisi kama TANESCO anapewa namba hiyo na kwenda kulipia ili kuunganishiwa umeme, akishalipa anapokea risiti ya kielektroniki na anasubiri huduma na kwamba hakuna ubabaishaji wakiwamo vishoka.

Anasema kuwa hiyo ni hatua ya kuenza jitihada za Nyerere kuifanya nchi ijitegemee kikamilifu kwa mapato yatokanayo na rasilimali zake za ndani.

"Ni jambo ambalo linadhibiti fedha na kupunguza ufisadi na upotevu wa pesa za serikali kitu ambacho Nyerere hakukikubali. Hela ziliishia kwenye mikono ya wachache. Risiti zilifojiwa na pesa hazikuingia pale zilipotakiwa kufikishwa." Anasema Monyo.

Anaongeza kuwa upotevu wa mapato ulizidi hasa pale maofisa wasio waaminifu walipokuwa na vitabu binafsi vya risiti wakati walitakiwa kutumia vya serikali."

"Ni jambo ambalo linadhibiti fedha na kupunguza ufisadi na upotevu wa pesa za serikali kitu ambacho Nyerere hakukikubali. Hela ziliishia kwenye mikono ya wachache. Risiti zilifojiwa na pesa hazikuingia pale zilipotakiwa kufikishwa." Anasema Monyo.

**FAIDA ZAKE**

Monyo anasema kuwapo kwa namba hizo kunarahisisha kazi za ofisi ya udhibiti na ukaguzi wa fedha za serikali kwa vile kazi yao itafanyika kielektroniki na kupunguza madai ya fedha kutumiwa bila kuwa na maelezo sahihi.

Aidha, anasema inaweza kuwa ni njia bora ya kupunguza matumizi na gharama kubwa za ukaguzi wa hesabu za serikali.

Dokta Kamugisha Byabato, kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine Tanzania -Mwanza, ambaye ni mhandisi wa nishati na masuala ya uchumi, akizungumzia 'kontroli number' anasema enzi za Nyerere kodi zilikuwa kidogo kwa kuwa serikali ndiyo ilikuwa ikitoa huduma zote bila kulipiwa.

Hata hivyo, wafanyabiashara na vitega uchumi vya kulipa kodi, vilikuwa vichache, aidha, mashirika ambayo yalitarajiwa kufanya biashara na kuipa serikali gawiwo lakini pia kujiendesha yenyewe hayakufanya hivyo badala yake yalikuwa yakiinyonya na kuifilisi nchi kwa kupewa ruzuku.

"Ndiyo maana serikali ya awamu ya tatu iliyobinafsisha ili kuondoa mzigo wa ruzuku kwa mashirika na kampuni yasiyokuwa na tija. Lakini leo, kwa kutumia teknolojia ya 'control number' kulipia malipo yote ya serikali, mashirika na wakala yanalipa gawiwo." Anasema Dk. Byabato.

Anasema njia hiyo ambayo wakati wa uhai wake isingewezekana kwa sababu kutokuwepo teknolojia na kompyuta inatumika leo kwenye kukusanya mapato kwenye vitega uchumi alivyoanzisha mfano bandari, forodha (leo TRA), Shirika la Reli (TRC) na TANESCO.

Leo, ofisa hashiki pesa mkononi, si rahisi kukimbia na pesa, serikali imedhibiti ujanja na upotevu wa mapato uliokuwa unafanyika kiholela kutokana kughushi risiti na kukwepa kodi," anasema mtaalamu.

Mafanikio ya kutumia teknolojia hiyo wakati huu wa kuenzi mchango wa Nyerere kwenye kuongeza mapato ya taifa kwa ajili ya maendeleo ya nchi, anayataja kuwa ni ongezeko la juu la kodi lililofikia takribani Shilingi trilioni 1.3 kwa mwezi. Yote hayo, huifanya nchi kutumia fedha za ndani kwenye miradi ya kijamii na kiuchumi.

**CHANGAMOTO**

Monyo na Dk. Byabato wanataja changamoto kubwa za teknolojia hiyo kuwa kutegemea mtandao wa intanet na pale ambapo hakuna huduma hiyo haiwezekani kulipa kupitia 'control number'.

"Ni lazima uwepo mtandao inaweza kuwa kero kwa wananchi wanaolazimika kwenda kufuata mitandao ili kulipia huduma TRA, TANESCO ... Inaweza kuwa kero kwa wanaokaa vijijini watalazimika kuifuata huduma mijini." Anasema Monyo.

Mtaalamu huyo wa mahesabu anasema kuwa inaweza kuongeza gharama zaidi iwapo ofisi za malipo kwenye miji au maeneo jirani na vijiji hayatakuwa na huduma ya mtandao ya kuaminika.



Mwalimu Nyerere akitafakari masuala ya maendeleo . **PICHA: MTANDAO**

NYERERE ALIPOWALILIA WATANZANIA ....

# Kuuishi wosia huu wa Baba wa Taifa ndiko kuipenda Tanzania



Viongozi na wananchi wakizuru kaburi la Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kijijini kwake Butiama, Mara. **PICHA: MTANDAO**

**Na John Mapepele, SINGIDA**

"NINAJUA nitakufa, sitapona ugonjwa huu... ninawaacha Watanzania wangu, najua watalia sana, nami nitawaombea kwa Mungu. Ninaondoka nikiwa nimewaachia taifa moja, lenye umoja na amani. Wosia wangu kwao;, waipende nchi yao kama wanavyowapenda mama zao. Wajue hawana nchi nyingine zaidi ya Tanzania". Huu ni ujumbe wa mwisho wa hayati Mwalimu Julius Nyerere kabla ya kuaga dunia Oktoba 14 , 1999 kwenye hospitali ya Mtakatifu Thomas nchini Uingereza.

Tanzania inaadhimisha kumbukumbu ya miaka 21 tangu kufariki Baba wa Taifa aliyekuwa akisumbuliwa na maradhi ya Saratani ya damu na kuzikwa kijijini kwao Mwitongo Butiama mkoani Musoma.

Wakati wa msiba wa Baba wa Taifa nilikuwa masomoni kwenye Chuo Kikuu cha Tumaini Mjini Iringa, nilikoshuhudia Iringa na Tanzania ikigubikwa na simanzi na majonzi kwa takribani wiki mbili, ambayo sasa imebaki kuwa kumbukumbu ya maisha.

Sikumfahamu Mwalimu Nyerere zaidi ya kumsoma vitabuni na kumwona kwenye vyombo vya habari na pengine ni miezi minne kabla ya kifo chake alifika Kalenga mkoani Iringa kushiriki mazishi ya aliyekuwa Spika wa Kwanza marehemu Adam Sapi Mkwawa, Juni 28, 1999. Aliongea kwa kifupi na kutoa masikitiko yake kwa kifo Sapi Mkwawa.

Kabla ya kujitosa kwenye siasa alikuwa mwalimu, tasnia ambayo ilimpa jina lililomtambulisha duniani kote. Alijiuzulu ualimu na kuzunguka nchi nzima kuzungumza na watu wa kawaida na machifu ili kuleta umoja katika kupigania uhuru.

Nyerere ndiye mwasisi wa itikadi ya ujamaa na kujitegemea iliyotangazwa na Azimio la Arusha maka 1967

Mwanamapinduzi huyu aliongoza Tanganyika kwanza 1961 hadi 1964 kama Waziri Mkuu, baadaye Rais na baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, aliendelea kuwa Rais wa Tanzania kuanzia 1964 hadi mwaka 1985.

Philipo Mangula, Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara akiwa Singida hivi Karibuni anamwelezea Nyerere kuwamba alikuwa kiungo katika Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kutengeneza Tanzania mara baada ya mapinduzi ya Zanzibar ya 1964.

Ndiye Februari 5, 1977 aliongoza muungano wa TANU Afro Shirazi cha Zanzibar kuanzisha chama kipya cha CCM na akawa mwenyekiti wa kwanza.

Nyerere ni kati ya viongozi wachache wa Afrika ambao wameacha madaraka kwa hiari baada ya kutawala kwa muda mrefu akiwa bado anapendwa na wananchi walio wengi.

> Suala la udini na ukabila ni mambo nyeti ambayo Mwalimu Nyerere aliyazungumzia katika hotuba nyingi alizowasilisha na kuzungumzia umuhimu wa umoja na uhuru wa kuabudu kipindi hiki Rais Magufuli amewaunganisha waumini na viongozi wa dini na madhehebu yote kumwomba Mwenyezi Mungu kuiepusha nchi na corona.

Alipostaafu uongozi 1985 na kumpisha Ali Hassan Mwinyi kuiongoza Tanzania, alirudi kijijini kwake Butiama na kuanza kilimo. Hata hivyo aliendelea kuongoza CCM hadi 1990 na kubaki kuwa mwanasiasa nguli hadi hadi kifo chake.

**MAFANIKIO YAKE**

Moja ni kujenga umoja wa taifa kati ya watu wa makabila na dini tofauti, na hivyo kudumisha amani ya muda mrefu tofauti na hali ya nchi nyingine za Afrika.

Ni kutokana na mafanikio hayo Kanisa Katoliki lilianzisha mchakato wa kumtangaza Mtumishi wa Mungu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuwa mwenye heri na hatimaye Mtakatifu.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, anamwelezea kuwa mkombozi kwa kutoa mchango kwa vyama vya ukombozi vya Kusini mwa Afrika kama vile Zimbabwe Afrika Kusini , Namibia, Angola na Msumbiji.

Rais John Magufuli ni miongoni mwa viongozi wanaojipambunua kwa namna ya kipekee kufuata nyayo na misingi ya Baba wa Taifa katika masuala kadhaa ya uongozi kama siasa na uchumi.

Katika suala la uongozi Mwalimu alisisitiza nidhamu na maadili ya uongozi akisema "inatakiwa ukiulizwa swali kwamba huyu atapiga vita rushwa? Jibu litoke ndani ya moyo. Nchi yetu ni masikini bado haijawa ya matajiri hivyo tunataka tuendelee kushughulika na umaskini wetu na matatizo ya wananchi, tunataka nchi yetu ipate kiongozi safi", alisisitiza Mwalimu

Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais Magufuli inakemea kwa nguvu zote mafisadi na wala rushwa ambao wamechukuliwa hatua za kisheria.

Kwenye kupambana na ujinga, maradhi na umaskini, Mwalimu Nyerere alisisitiza kuwa kama Tanzania itafanikiwa kuyamaliza itakuwa miongoni mwa nchi itakayoendelea zaidi duniani.

Aidha, Rais Magufuli ameelekeza fedha nyingi kwenye maeneo ya kimkakati kama ujenzi wa vituo vya afya, miundombinu, na kugharamia elimu lakini pia ametimiza ndoto ya Mwalimu Nyerere ya kuhamishia makao makuu ya nchi Dodoma.

Suala la udini na ukabila ni mambo nyeti ambayo Mwalimu Nyerere aliyazungumzia katika hotuba nyingi alizowasilisha na kuzungumzia umuhimu wa umoja na uhuru wa kuabudu kipindi hiki Rais Magufuli amewaunganisha waumini na viongozi wa dini na madhehebu yote kumwomba Mwenyezi Mungu kuiepusha nchi na corona.

Akihutubia wananchi kwenye kampeni Kinyerezi Dar es Salaam hivi karibuni Rais Magufuli anasema Tanzania inasimamia misingi iliyoachwa na Baba wa Taifa na kusisitiza kuwa inamwamini Mwenyezi Mungu.

"Tanzania ina Mungu kwa sababu anatusikia. Na katika kipindi cha corona uchumi wetu ulizidi kupaa hata kutangazwa kuwa nchi ya uchumi wa kati. Hongereni Watanzania kwa kushikamana" anaongeza Rais Magufuli.

Nyerere alikemea ukabila kila wakati alipozungumza na hakutaka kabisa kuwe na maswali kama wewe ni kabila gani? Ni katika hilo alifanikiwa kwa kiasi kikubwa, si kwa kawaida nchini Tanzania kuulizana kuhusu masuala ya ukabila.

Hayo ni baadhi ya mambo aliyokuaakisisitiza Mwalimu Nyerere katika hotuba zake, lleo Watanzania wapoadhimisha miaka 21 ya kifo cha Baba wa Taifa bado falsafa zake zinaendelea kuishi.

Lakini jambo kubwa zaidi ni hili, falsafa zake zinaendelea kuishi katika kipindi hiki cha kampeni za uchaguzi mkuu wa kuchagua Rais, wabunge na madiwani ambapo ifikapo Oktoba 28 wananchi watapiga kura kwa viongozi ambao watawaongoza kwa miaka mingine mitano 2020-2025.

Wakati leo Tanzania inamuenzi ni muhimu kwa wapiga kura kujua thamani yao ya kutumia haki yao ya msingi ya kuwachagua viongozi watakaowaletea maendeleo huku wakikumbuka wosia wa Baba wa Taifa alioutoa katika kipindi kifupi kabla ya kuaga dunia Oktoba 14, mwaka 1999 kwenye Hospitali ya Mtakatifu Thomas nchini Uingereza kuwa:

"Ninajua nitakufa, sitapona ugonjwa huu... ninawaacha Watanzania wangu, najua watalia sana, nami nitawaombea kwa Mungu. Ninaondoka nikiwa nimewaachia taifa moja, lenye umoja na amani. Wosia wangu kwao;, waipende nchi yao kama wanavyowapenda mama zao. Wajue hawana nchi nyingine zaidi ya Tanzania".

MIAKA 21 BILA NYERERE:

# ALIDUMISHA MAISHA KAWAIDA KUPINDUKIA AKIWASHANGAZA WAGENI, KWAKE NI 'POA'

## • Ushuhuda wa Msasani aina yake

**Na Hilal Sued**

LEO imetimia miaka 21 tangu kututoka mwasisi wa Taifa na Rais wa kwanza, Mwalimu Julius Nyerere, aliyefariki katika hospitalini nchini, Uingereza Oktoba 14 1999.

Ni maadhimisho kitaifa, ikiwa wiki mbili kamili kabla ya kufanyika Uchaguzi Mkuu nchini, unaonendana na ushindani mkubwa.

Daima siishiwi kuhoji kukosekana viongozi bora wa kutosha barani Afrika, wenye uzalendo na wako kinyume na wanaoingia madarakani kujilimbikizia mali kwa manufaa binafsi.

Maana hapo pia ndio huzaa usemi "Penye miti hukosa wajenzi." Utajiri wa rasilimali za Afrika, inapotokea kwamba inatumika vibaya.

Ni mtazamo ambao ukiletwa ndani ya nchi, kikubwa ambacho Mwalimu Nyerere amewaachia Watanzania, mbali na ukombozi kutoka makucha ya ukoloni, kuna hilo la maadili na heshima ya nchi duniani.

Iko wazi wote wanakumbuka namna alivyochukia udhalilishaji wa aina zote dhidi ya wananchi wake kwamba dhana ya kiadui.

Kuna wakati alilazimika kuwatimua wageni waliofika nchini, kwa kazi au kuwekeza (yaani kufanya biashara -- kama ilivyokuwa ikiitwa siku hizo) ilipobainika ama walitukana au kunyanyasa wananchi wazalendo na kuna mara kadhaa alifanya hivyo kwa kuwapa saa 24 waondoke nchini

Mwalimu Nyerere, alilinda heshima ya mwananchi, katika mtazamo na sababu mwenyewe aliwaongoza wananchi wake kwa uadilifu mkubwa na hapakushuhuduiwa makuu, ikiwamo ama simulizi au tetesi ya kujilimbikizia mali.

Alifanya hivyo ikiwa ni mfano kwa viongozi wenzake na hata akisisitiza kuwawekea miiko ya uongozi chini ya Azimio la Arusha ya mwaka 1967 ambayo ilitafsiriwa "tamko rasmi la nchi itakavyooonizwa kwa kutumia Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea."

Ni kwamba, Mwalimu Nyerere alijua mamilioni ya Watanzania walikuwa masikini, hivyo viongozi wangejiingiza katika kujilimbikizia mali, kulikuwapo uwezakano mkubwa wa kuwasahau wananchi hao.

**UKWELI WAKE**

Hakuna amjuaye vyema, anayethubutu kupinga ukweli Mwalimu Nyerere, alikuwa mbali na ulimbikizaji mali, katika maisha yake na familia.

Uzoefu wangu binafsi, mara ya kwanza kabisa nilifika nyumbani kwakeMsasani mwaka 1992, akiwa tayari nu mstaafu katika uongozi wa nchi.

Nilikuwa mwandishi katika gazeti la Kiingereza la kila wiki, miongoni mwa magazeti ya kwanza yaliyoanzishwa baada ya tasnia ya upashaji habari iliporuhusiwa kuwa huria.



Mwalimu alituita wanahabari kuzungumzia hoja ya kikundi cha Wabunge kilichoitwa G55, kikishinikiza hoja ya kuwapo serikali ya Tanganyika.

Baada ya mchakato wa usajili wa majina getini nyumbani kwake, tulielekea kwenye jengo la ghorofa moja. Lilikuwa la kawaida sana, inayoelezwa linatokana na mkopo wa benki, alipokuwa bado Rais.

Tathmini binafsi, niliiweka katika majengo mengine yanayopatikana kwa namna hiyo wakati huo jijini Dar es Salaam, katika maeneo kama Magomeni, Ilala au Mwanayamala, ambalo mpita njia hana sababu ya kulitupia macho ya mshangao.

Wakati tukielekea kufikia jumba hilo jirani na getini, niliona nyasi upande wa njia hiyo hazikuwa zimekatwa na eneo lote lilikuwa na ukimya mkubwa.

Hata hivyo, nikajipa tafsiri makazi ya rais huwa si eneo la shughuli kubwa, hasa kwa huyu aliyekuwa kastaafu mwaka wa saba. Nikajipa ahadi "subiri, kuna mengine…."

Kufika kwenye jengo hilo, wengi wageni tulishtushwa kukuta baadhi ya vioo vya madirisha ya luva (louvers), ambayo yalitawala wakati huo vimevunjika na sehemu nyavu za kuzuia mbu zimechanika, huku rangi ya kuta imepauka.

Binafsi nikahamisha imani kwamba huenda hapo ni pa wasaidizi na makazi halisi yalikuwa nyuma ya jengo.

Lakini ghafla, fikra hizo zilifutika baada ya kukaribishwa kwenye veranda yenye sakafu ya 'terrazzo' huku bahari ya Hindi ikionekana kwa mbali.

Kutokana na picha nilizokuwa nikiziona katika magazeti ni zama hizo, ndiyo sehemu alikokuwa anakutana na kuongea na viongozi mashuhuri duniani wakati wa uongozi wake.

Baada ya muda, tukatangaziwa ujio wa Mwalimu Nyerere, tukimuona anateremka ngazi kutoka ghorofani, aliyefuatana na Katibu Muhtasi wake wa miaka mingi, Bi Joan Wickens, aliyekuwa na asili ya Uingereza na msaidizi wake mwingine wa kiume.

Alifika na kutupa mikono wote. Nami ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kupeana mkono na akatuashiria kuketi. Viti havikutosha, baadhi ilibidi tusimame. Yeye aliliketi katika kiti chake cha bembea akiupa mgongo Bahari ya Hindi.

Kuna baadhi yetu walipata bahati ya kukaa katika sofa kama vitatu, viti ambavyo, pamoja na kile kiti cha bembea, vilikuwa 'vimechoka.'

Ni viti vya kihistoria, maana watu mashuhuri duniani kama Dk. Henry Kissinger, Kenneth Kaunda, Gamal Abdel Nasser, Indira Gandhi na Fidel Castro walishakalia sofa hizo.

Baada ya kuketi, mkutano ulianza huku binafsi mawazo yangu yalihama kabisa, nikijaribu kuyatuliza akilini niliyoyaona.

Nikajiulize "Ilikuwaje mtu huyu maarufu, shujaa wa ukombozi wa Bara la Afrika, na ambaye hata baada ya kustaafu uongozi, aliendelea na umaarufu wake kwa kushikilia msimamo wake wa uongozi wa kimaadili na visheni yake ya Ujamaa, kuridhika kuishi katika mazingira duni kama haya?"

Bila shaka mazingira aina hiyo, ndiyo aliishi hata alipokuwa Rais, tabia inayoeleza jinsi Mwalimu Nyerere alivyowapiku viongozi wengi sana Barani Afrika na pengine duniani, katika uadilifu na kujinyima.

Kwa vipi alikataa maisha ya anasa, kitu ambacho angeweza kukipata wakati wowote kwa ishara ya vidole tu?

Wakati nikimsikiliza Mwalimu akitoa mashambulizi yake dhidi ya kikundi cha G55, aliyokieleza kinadhamiria kuuvunja Muungano, akiilaani kwa matamshi labda hiyo itokee juu ya kaburi lake.

Huku mimi nilibaki napandwa na simanzi zenye ghadabu, kulikoni viongozi aliowakabidhi madaraka waliamua kuyatelekeza makazi yake katika hali hii?

Siku ya pili, habari kubwa katika magazeti haikuwa kuhusu kile Mwalimu Nyerere alichokieleza kuhusu 'Tanganyika,' bali hali ya makazi yake, nikiamini ni habari ambayo hata yeye ilimshitua.

Ni habari zilizopokewa na serikali kwa haraka na namna chanya, timu ya mafundi iliotunga mahali hapo na kazi kubwa ya ukarabati ilifanyika.Matokeo ya kazi hiyo ilishuhudiwa ndani ya wiki tatu.

**SAFARI YA PILI**

Baadaye nilifika hapo katika makazi hayo kwa ajili ya mazungumzo maalum kikazi na msaidizi wa Mwalimu, Mama Wickens, iwapo Mwalimu anakubaliana na uamuzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuipa Barabara ya Pugu (Pugu Road) jina lake yaani 'Julius Kambarage Nyerere Road.'

Wakati huo, Mwalimu Nyerere alikuwa kijijini kwao Butiama, Mara na baada ya muda Mama Wickens (bila shaka baada ya kuwasiliana naye kwa simu) akanijibu kwamba "Rais mstaafu hataki jina lake lipewe jina la barabara au kitu chochote kile wakati akiwa bado hai."

Hivyo, Halmashauri ya Jiji Dar es Salaam, ililiondoa kwenye alama za barabara na kubakia 'Nyerere Road' kwa mtazamo kina Nyerere walikuwa wengi waliozaliwa humu duniani.

Ni baada ya ukimya mrefu, baadaye waombolezaji waliofika nyumbani kwake mara tu baada ya kufariki kwake mwaka 1999, walishangaa kuona nyumba katika hali isiyoridhisha, huku wakiwaona mafundi wanafanya maboresho dhidi ya hali hiyo.

Ni mazingira yanayofungua maswali, leo hii ni viongozi wangapi wanaishi katika nyendo hizo? Maana, kuna baadhi wanadaiwa kuishi katika maisha ya pepo na anasa kubwa, tofauti kabisa na ushuhuda kutoka kwa Mwalimu Nyerere.

**FAMILIA**

Bado nakumbuka zaidi ya miaka 40 iliyopita, nikiwa nafanya kasio jijini Arusha, nakumbuka tukio la mtoto wa Mwalimu Nyerere, aliyekuwa akisoma shule mojawapo ya bweni, Mkuu wa Mkoa wakati huo, Abdul-Nuru Suleman (sasa marehemu) alihisi mtoto huyo anapata adha kuishi shuleni.

Aliamua kumhamisha na kumuweka nyumbani kwake, huku gari la serikali likimpeleka shuleni na kumrudisha kila siku. Mwalimu Nyerere alipopatiwa habari hizo, alicharuka sana dhidi ya upedeleo huo na aliamrisha mtoto huyo arudi bwenini kwa haki na adha ya kujichanganya na wenziwe.

Hivyo ndivyo alivyoishi na wanawe katika usawa na watoto wa wananchi wengine, hali iliyotawala hata itifaki nyingine katika tiba, akithamini vya nyumbani,

Huko nyumbani Msasani na Butiama, Mwalimu Nyerere, katika maisha yake ya ustaafu amekuwa mtu wa kujhudumia mahitaji madogo kama huduma za ndani na kwenda shamba.

Alipohamia nyumbani kijijini Butiama, alikuwa mcheza bao maarufu, mshindani wake mkuu akiwa binamu na rafiki yake marehemu Mzee Nyang'ombe Warioba, kutoka kijiji jirani cha Muryaza.

***MWENYEZI MUNGU AIWEKE ROHO YAKE MAHALI PEMA. AMINA.***





# Bil. 2.4/- kuchimba visima pembezoni mwa jiji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), imeanza kuchimba visima vya maji maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dodoma vitakavyogharimu Sh. bilioni 2.4 ili kutatua uhaba wa maji uliopo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kwenye eneo mojawapo linalochimbwa visima vitano, eneo la Ihumwa, Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi David Pallangyo, alisema kutokana na ujio wa serikali Dodoma mahitaji ya maji yameongezeka kwa kiasi kikubwa na kusababisha upungufu katika baadhi ya maeneo.

Alisema uchimbaji wa visima hivyo pembezoni mwa mji, ni mpango wa muda mfupi wa kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo wakati wakisubiri utekelezaji wa miradi mikubwa ambayo itahudumia wananchi kwa miaka ijayo.

**Hili ni moja ya eneo ambalo tutatengeneza visima kadhaa vya kuzalisha maji ili kuongeza uzalishaji wa maji ambapo kwa mjini mahitaji ni makubwa.**

"Hili ni moja ya eneo ambalo tutatengeneza visima kadhaa vya kuzalisha maji ili kuongeza uzalishaji wa maji ambapo kwa mjini mahitaji ni makubwa," alisema.

"Tutatoa maji hapa na kuyapeleka hadi mjini, ili kupunguza tatizo la maji eneo la mjini, vitachimbwa visima vinavyozalisha si chini ya mita za ujazo elfu 3,000 kwa siku zitakazosaidia maeneo ya Mwangaza, Njedengwa, Ihumwa na mengine ya Mjini," aliongeza.

Alibainisha kuwa kuna maeneo mengine ya pembezoni pia visima vitachimbwa, lengo ni kuhakikisha huduma ya maji inaimarika.


Akikagua kisima hicho, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, alisema serikali kupitia wizara hiyo, imetoa Sh. bilioni moja kati ya Sh. bilioni 2.4 zilizoombwa na DUWASA kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji katika maeneo yenye uhaba wa maji.

Alisema hatua hiyo ni kutokana na ongezeko la mahitaji ya huduma ya maji katika meneo mbalimbali ya jiji hilo hasa ya pembezoni.

Mhandisi Sanga alisema kuwa serikali ina mipango ya muda mfupi, ya kati na muda mrefu ya kutatua kero hiyo.

"Mipango ya muda mfupi ni kama ujenzi wa visima vya dharura katika eneo la Ihumwa na mipango ya muda wa kati ni ujenzi wa bwawa la Farkwa na muda mrefu ni kutoa maji Ziwa Victoria," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alipongeza uongozi wa DUWASA kwa kutatua kero za maji kwa jiji na kuwataka kuongeza ushirikiano ili kufikia malengo.




Mkazi wa Kisasa jijini Dodoma, Baraka Shibanda (kushoto), akipokea zawadi ya dola za kimarekani 100 kutoka kwa mshauri wa kampuni ya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni ya Fx Hedging Victory, Manyiri Isaack, baada ya kuhudhuria mafunzo ya kuwajengea uwezo vijana kuhusu biashara yaliyofanyika jijini humo jana. Katikati ni mkurugenzi wa kampuni hiyo, Victor Maeda. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ahamasisha wamachinga kupiga kura

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, amewaomba viongozi wa wafanyabiashara wadogo kuhamasisha waliojiandikisha kupiga kura kujitokeza kwa wingi Oktoba 28, mwaka huu, ili kuchagua viongozi bora.

Yuna aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na viongozi wa masoko ya wafanyabiashara hao katika kikao cha tathmini ya utendaji kazi zao na kupitia Katiba yao.

Alisema viongozi hao hao wana wajibu wa kuhamasisha wenzao wenye vitambulisho vya kupigia kura kutumia fursa hiyo kujitokeza kwa wingi ili kuchagua wagombea watakaowafaa kuwaleta maendeleo.

"Kura yenu ni sauti yenu, msifanye makosa ambayo yatawagharimu kwa miaka mitano ijayo kwa kuwapigia kura viongozi wanaoigiza kwa kutaka uongozi wakati hawana sifa ya kuongoza," alisema.

"Ninawaomba tumieni fursa ya kupiga kura, kwa maslahi ya Watanzania na siyo kwa ushabiki wa chama cha siasa, mkifanya hivyo mtajikuta mnajutia kwa kipindi chote cha miaka mitano," alisisitiza.

Pia aliwataka kutoa elimu kwa wajasiriamali juu ya kufanya biashara kwenye maeneo rafiki ambayo hayahatarishi maisha na bidhaa zao.

Ofisa huyo alisema bado kuna tatizo kwa baadhi ya machinga kufanya shughuli zao kwenye maeneo hatarishi, jambo ambalo ni ukiukwaji wa taratibu za jiji.

Alisema wengi wao wanapanga kwenye barabara na njia za watembea kwa miguu, bila kujali hatari itakayojitokeza.

Naye Katibu wa Umoja wa Wamachinga Wilaya ya Dodoma Mjini, Anna Charles, alisema wafanyabiashara hao wana kila sababu ya kujitokeza kupiga kura kwa kutambua ni haki yao kikatiba.

# Mpango kuendeleza mazao kilimo waanza

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imezindua mpango wa kuendeleza viwanda vya mazao ya kilimo utakaochochea uchumi wa viwanda hapa nchini na kuwanufaisha wakulima.

Mpango huo umeandaliwa na Taasisi ya Kuendeleza Kilimo Afrika (AGRA) ili kusaidia kuinua sekta ya kilimo.

Akizungumza jana kwenye uzinduzi huo, Katibu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe, alisema mpango huo umelenga kutafuta fedha kwa ajili ya kusaidia viwanda hivyo ili Tanzania iendelee kupiga hatua zaidi kiuchumi.

"Tunashukuru AGRA kwa kuandika andiko la mpango huu ambalo tunaamini litakuwa na tija katika uchumi wa nchi yetu," alisema Prof. Shemdoe.

Aidha, Prof. Shemdoe alisema kuwa andiko hilo litasimamiwa kupitia programu ya kuendeleza sekta ya kilimo awamu ya pili (ASDP II).

Alisema mpango huo unatarajiwa kuleta matokeo chanya na kuongeza faida katika sekta ya kilimo nchini.

"Tunatakiwa kuendelea kukaa katika nchi zenye uchumi wa kati kwa kujenga viwanda vitakavyosaidia kuongeza ajira kwa vijana wanaohitimu kutoka vyuo mbalimbali hapa nchini," alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alisema kuwa kupitia mpango huo serikali inatarajia kufanya mapinduzi ya viwanda ili kuwa na tija nchini.

Kusaya alisema kuwa mpango huo ukitekelezwa tatizo la ajira hapa nchini litakuwa historia kwa kuwa viwanda vingi vikijengwa vitasaidia kuondoa tatizo hilo.

Aidha, Kusaya alisema tayari Wizara ya Kilimo imeshaanza kufufua Viwanda vya Kilimo katika Mkoa Geita na Wilaya ya Chato ambavyo vilikuwa vikichakata pamba.

"Wizara itaendelea kuzindua hata viwanda vilivyosinzia lengo ni kuwa na viwanda vingi hapa nchini," alisema Kusaya.

Alisema serikali inaendelea kukuza sekta ya kilimo kwa kuzalisha mbegu bora, kutumia teknolojia za kisasa pamoja na kuongeza maofisa ugavi ambao watakuwa wakiwasaidia wakulima kulima kilimo chenye tija.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema mpango huo ni muhimu kwa taifa kwa kuwa lengo la Tanzania kufikia uchumi wa juu.

**Tunatakiwa kuendelea kukaa katika nchi zenye uchumi wa kati kwa kujenga viwanda vitakavyosaidia kuongeza ajira kwa vijana wanaohitimu kutoka vyuo mbalimbali hapa nchini.**





# Mil. 795/- zakarabati shule kongwe Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imetumia zaidi ya Sh. milioni 795 kukarabati miundombinu ya Shule ya Sekondari Mbeya ambayo ilijengwa zaidi ya miaka 59 iliyopita.

Shule hiyo ambayo ni miongoni mwa taasisi kongwe za elimu ya sekondari, ilikuwa haijawahi kufanyiwa ukarabati mkubwa tangu ilipojengwa na kusababisha baadhi ya majengo kuwa hatarishi kwa maisha ya wanafunzi.

Mkuu wa Shule hiyo, Magreth Haule, aliiambia Nipashe juzi kuwa shule hiyo ilijengwa mwaka 1961 wakati nchi ikipata uhuru na kwamba baadhi ya madarasa yalikuwa yamechakaa kupita kiasi.

Alisema ukarabati wa shule hiyo ulifanyika serikali ilipokuwa imezifunga shule na taasisi zote za elimu kama mojawapo ya hatua za kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona.

**Shule hiyo kwa sasa ina wanafunzi 1,447 kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha sita na kwamba kati ya wanafunzi hao, wavulana ni 688 na wasichana 759.**

Haule alisema kutokana na uchakavu wa miundombinu ya shule hiyo, kuliibuka matatizo mengine ikiwamo kukatika mara kwa mara kwa umeme pamoja na kuziba mifumo ya maji taka, hivyo kuongeza hatari kwa jamii.

"Kwa sasa baada ya ukarabati shule inapendeza na inatia moyo wa kufanya kazi maana vyoo vyetu vimeboreshwa, wanafunzi wanasoma kwa amani na hata walimu wameongeza ari ya kufundisha. Wametuwekea mpaka marumaru kwenye ofisi zetu," alisema Haule.

Alisema shule hiyo kwa sasa ina wanafunzi 1,447 kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha sita na kwamba kati ya wanafunzi hao, wavulana ni 688 na wasichana 759.

Mbali na idadi hiyo ya wanafunzi, alisema shule hiyo ina watumishi 80 ambao kati yao 71 ni walimu na tisa ni watumishi wasiokuwa walimu wakiwamo walezi wa wanafunzi, walinzi na wasaidizi wa ofisi.

Alisema shule baada ya kukarabatiwa, sasa ina matundu ya vyoo 76 ambayo kati yake 14 yanatumiwa na walimu tofauti na awali ambapo walikuwa wanatumia matundu matatu pekee kutokana na mengine kuziba.

Mkuu huyo aliishukuru serikali kwa kuikumbuka shule hiyo ambayo imetoa wasomi na viongozi mbalimbali akiwamo aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Nehemia Mchechu.

Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema mbali na ukarabati wa shule hiyo, pia perikali imekarabati shule zingine tatu kongwe za mkoa huo.

Alizitaja shule zingine kuwa ni Shule ya Ufundi ya Wavulana ya Iyunga, Shule ya Wasichana Loleza na Shule ya Sekondari Rungwe ambazo zote zimekarabatiwa ndani ya miaka mitano.

Chalamila alisema pamoja na miradi hiyo ya ukarabati wa shule kongwe, pia serikali imefanya maendeleo mbalimbali mkoani humo ikiwamo sekta ya afya, miundombinu ya barabara na kilimo.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mbeya, wakiwa kwenye mistari shuleni hapo jana, baada ya ukarabati wa miundombinu sasa wanasoma kwa uhuru tofauti na ilivyokuwa awali. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mgombea aahidi kusaidia wakulima

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa tiketi ya Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), Protas Mgimbila, amesema endapo atachaguliwa, atahakikisha anawasaidia wakulima wa viazi mviringo kuunda vyama vya ushirika ili kuboresha biashara ya zao hilo.

Mgimbila aliyasema hayo juzi alipokuwa anazungumza na wananchi wa Kata ya Iduda jijini Mbeya kwenye mkutano wa kampeni ambapo alisema vyama vya ushirika vitasaidia kuboresha biashara ya viazi.

Alisema moja kati ya vitu ambavyo wakulima hao watakuwa wameviepuka kwa kuunda ushirika ni pamoja na kukomesha uuzaji wa zao hilo kwa kutumia vipimo ambavyo wafanyabiashara wanavitumia kuwanyonya wakulima.

"Kwa sasa biashara ya lumbesa kwenye viazi vyetu inatutesa sana, hii inasababishwa na sisi kutokuwa na sauti ya pamoja kwenye biashara. Lakini tukijiunga kwenye vyama vya ushirika tutakomesha biashara hii ambayo mimi naiona ni haramu," alisema Mgimbila.

Alisema endapo atachaguliwa kuwa mbunge atahakikisha anawashawishi wabunge wenzake kutunga sheria ambayo itawabana wanunuzi kununua zao hilo kwa kutumia mizani badala ya kukadiria kwenye mifuko.

Alisema Jiji la Mbeya pamoja na hadhi yake, bado kuna baadhi ya kata zilizoko pembezoni ambazo ndizo uchumi wake unategemea kilimo cha viazi mviringo.

Vilevile alisema atahakikisha anawapigania wananchi wa maeneo hayo ili wajengewe barabara zinazowaunganisha na barabara kuu ambayo itarahisisha usafirishaji wa mazao hayo.

# Meneja aeleza utekelezaji miradi mikubwa maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UONGOZI wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Mbeya, umesema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, ulikabidhiwa na Serikali Kuu zaidi ya Sh. bilioni 160 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Meneja wa Tanroads Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Eliazary Rwekiza, aliyasema hayo juzi alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa miradi ya barabara iliyotekelezwa mkoani humo.

Alisema moja kati ya miradi ambayo imetekelezwa ni barabara ya Kikusya- Ipinda – Matema iliyopo wilayani Kyela yenye urefu wa kilomita 39.1 ambayo imejengwa kwa kiwango cha lami na imeshakamilika.

Alisema barabara hiyo imegharimu Sh. bilioni 65.8 na ulitekelezwa kwa muda wa miaka minne kuanzia 2015 mpaka 2019 na kwamba ulikuwa unatekelezwa na kampuni ya New Era International ya China.

Mradi huo, awali ulikuwa utekelezwe kwa muda wa miezi 18, lakini kutokana na matatizo mbalimbali ikiwamo mvua nyingi na ongezeko la kazi waliamua kuongeza muda zaidi.

"Awali barabara hii ilikuwa inaonekana ingekuwa na makalavati 16, lakini baadaye ikaonekana yatakuwa 20 na ndio maana mkandarasi akaongezewa muda lakini kwa sasa imeshakamilika kwa asilimia 100," alisema Rwekiza.

Aliutaja mradi mwingine kuwa ni ujenzi wa kituo cha pamoja cha forodha kati ya Tanzania na Malawi kinachojengwa katika mpaka wa Kasumulu, wilayani Kyela.

Rwekiza alisema ujenzi wa kituo hicho unaendelea chini ya Usimamizi wa TANROADS kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na kwamba unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 26.4.

Vilevile alisema kuna mradi mwingine wa ujenzi wa barabara ya Katumba –Mbambo Tukuyu wilayani Rungwe ambayo ina urefu wa kilomita 17 na unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 20.46.

Alisema mradi huo umegawanywa katika awamu mbili ambazo ni Bujezi-Mbambo kilomita 10 na Kibanja- Tukuyu kilomita saba ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami, ili kuunganisha Halmashauri za Rungwe na Busokelo kwa kiwango cha lami.

Barabara nyingine, kwa mujibu wa meneja huyo, ni ya Chunya-Makongolosi yenye urefu wa kilomita 39 na inatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 62 na kwamba barabara hiyo ina madaraja makubwa mawili ambayo ndiyo yanayochukua muda mrefu kukamilika.

"Vilevile tumepewa kazi ya kusimamia ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA), ambao serikali imetoa Sh. bilioni 18 kwa ajili ya kurekebisha runway (njia ya kurukia ndege) na kuweka taa," alisema Rwekiza.

Alisema mbali na miradi hiyo mikubwa pia ipo miradi mingine midogo midogo ambayo ofisi yake imekuwa ikisimamia na kwamba pia imegharimu fedha nyingi.

Aliwataka wananchi wa maeneo inakotekelezwa miradi hiyo kuitunza miundombinu ili idumu na kuwasaidia kwa muda mrefu kuinua uchumi wao.





# Mwinyi aahidi kufuta kodi zisizo na mashiko

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Mwinyi, amesema akichaguliwa kushika nafasi hiyo, ataondoa utitiri wa kodi na kuhakikisha wafanyabiashara wanapatiwa vitambulisho ili kufanya biashara zao bila bughudha.

Akizungumza na wafanyabiashara na wajasiriamali mbalimbali wakiwamo watembezaji watalii huko Kiwengwa, Kaskazini Unguja, alisema atazipatia ufumbuzi kero za wafanyabiashara kulipa kodi nyingi kwa mwaka, hivyo kuwaweka katika mazingira magumu.

**Malalamiko yenu nimeyapokea. Nikifanikiwa kuwa Rais, nakusudia kuondosha utitiri wa kodi na kuwawezesha kulipa kodi mara moja kwa mwaka.**

"Malalamiko yenu nimeyapokea. Nikifanikiwa kuwa Rais, nakusudia kuondosha utitiri wa kodi na kuwawezesha kulipa kodi mara moja kwa mwaka," alisema.

Dk. Mwinyi pia aliwataka watembezaji wa watalii katika ukanda wa Kaskazini Unguja kulitangaza jina zuri la Zanzibar ili wageni wengi zaidi wafike Zanzibar na serikali kupata mapato. Baadhi ya wajasiriamali wanaofanya biashara za bidhaa mbalimbali kwa watalii katika ukanda wa Kiwengwa walimwomba mgombea huyo kujenga mazingira mazuri ya biashara zao na kuondosha kodi nyingi wanazotozwa kwa mwaka.

"Sisi wafanyabiashara tuliopo Kiwengwa bado hatujafaidika na kufanya shughuli zetu za biashara kwa sababu tunakabiliwa na kodi nyingi tunazotozwa na halmashauri za wilaya," alisema Juma Said.

Dk. Mwinyi alifanya ziara ya kuwatembelea wajasiriamali wakiwamo kinamama wanaofanya kazi za kuanika dagaa pamoja na mamalishe kwa ajili ya kusikiliza kero zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao.



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCM, Dk. Hussein Mwinyi (mwenye miwani), akizungumza na wajasiriamali wa sekta ya utalii katika eneo la Kiwengwa Kaskazini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanawake wasuasua kugombea uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KURUGENZI wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Thabit Idarous Faina, amesema licha ya harakati mbalimbali za kuwahamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi, bado idadi ya waliojitokeza ni ndogo kulinganisha na wanaume.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua mkutano wa wamiliki wa vituo vya utangazaji kuhusu mwongozo wa kuripoti habari za uchaguzi. Mkutano huo ulifanyika katika ofisi za ZEC, Maruhubi.

Faina alisema wanawake waliogombea nafasi ya uwakilishi majimboni ni 61 kati ya wagombea 252 waliochukua fomu ZEC.

Alisema vyombo vya habari vina wajibu wa kuwahamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi majimboni na wasiwaachie wanaume pekee yao.

"Kwa nafasi ya udiwani wanawake 82 tu ndio waliogombea kati ya wagombea 360 waliogombea nafasi hiyo," alisema.

Alisema katika wagombea 17 wa nafasi ya urais wa Zanzibar waliopitishwa na tume ya uchaguzi, hakuna mwanamke na nafasi hizo zimegombewa na wanaume pekee.

Mkurugenzi huyo aliwataka waandishi wa habari kuacha kujihusisha kutoa habari za uchonganishi katika kipindi hiki cha kampeni za uchaguzi mkuu.

Alivitaka vyombo vya habari kutoa habari bila ya upendeleo ili kuwa na uchaguzi wa amani.

"Ni vyema waandishi wa habari kuzingatia kanuni na maadili ya taaluma yenu na kuripoti habari bila ya upendeleo," alisema.

Akiwasilisha mada ya vyombo vya habari na uchaguzi mkuu, mwanasheria kutoka ZEC, Khamis Issa Khamis, aliwataka waandishi wa habari kutoa taarifa za wagombea wa vyama siasa bila upendeleo.

Mwanasheria huyo alikipongeza kituo cha runinga na ITV kutoa taarifa zao kwa wagombea wote wa vyama vya siasa wakati huu wa kampeni bila upendeleo na kuviomba vyombo vyengine kuiga mfano huo.

Kuhusu matokeo ya uchaguzi alisema sheria ya uchaguzi imeweka kizuwizi mtu yoyote kutangaza matokeo bila ya tume ya uchaguzi kutangaza matokeo hayo.

Alisema endapo chombo chochote cha habari kitatoa matokeo bila tume kutangaza, kitatozwa faini ya Sh. milioni 50 na kwa mgombea atakayetoa matokeo, atatakiwa kulipa faini Sh. milioni 100 na kwa mtu mwengine wa kawaida atakayefanya hivyo, anaweza kufungwa jela miezi sita.

# Ahimiza kuwatumia watumishi wastaafu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Dk. Idrissa Muslim Hija, ameitaka Ofisi ya Mrajis wa Elimu kuendelea kushirikiana na kuwatumia wastaafu ili kuleta maendeleo katika ofisi yao.

Alisema ni utaratibu wa kisheria mfanyakazi kumaliza kulitumikia taifa, lakini kuna uwezekano wa kuendelea kuwatumia wafanyakazi hao kadri wanavyohitajika katika kuleta maendeleo nchini.

Akizungumza kwa niaba yake katika hafla ya kuwaaga wastaafu katika ofisi ya mrajis wa elimu waliomaliza muda wao wa kuitumikia serikali, katika ukumbi wa Wizara ya Elimu, Mazizini, mjini Unguja, Mkurugenzi wa Elimu ya Watu Wazima, Mashavu Ahmada Fakih, alisema ushirikiano mzuri ndio pekee unaoweza kuleta maendeleo.

Mashavu aliwataka kuwa tayari kufundishana kazi zao ili kukasimu madaraka mmoja anapoondoka kwa lengo la kuhakikisha kazi zinaendelea bila kuonekana upungufu wowote katika kazi.

Pia aliwataka kuhakikisha wanafuata sheria na kanuni za kazi pamoja na kufuata mazuri yote yalioachwa na wastaafu hao ikiwamo kufanya kazi kwa kujitolea, nidhamu za kazi na uaminifu wa hali ya juu ili kuleta maendeleo katika nchi.

Mkurugenzi huyo aliwataka wafanyakazi hao kuacha kufanya kazi kwa mazoea na tabia hiyo haiwezi kuwaletea mafanikio katika kazi zao na taifa, hivyo kuwa tayari kuwajibika kwa ushirikiano mzuri ili kupatikana kwa maendeleo.

Hata hivyo, aliiagiza ofisi hiyo kuhakikisha wanawaandalia vyeti maalum vya wastaafu hao kuonyesha kuwajali kutokana na utumikiaji wao wa kazi katika serikali ikiwa pia ni miongoni mwa kanuni za utumishi wa umma.

Naye Kaimu Mrajis wa Elimu Zanzibar, Thneyuu Mabrouk Hassan, aliwapongeza wastaafu hao kwa kuitumikia serikali kwa usalama na uzima na afya na kuwaomba kuwa tayari kuendelea kutoa michango na mawazo yao kadri watakapohitajika kwa lengo la kuleta maendeleo.

Mkurugenzi wa Utumishi na Uendeshaji Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Siajabu Suleiman Pandu, aliwaomba wafanyakazi kuhakikisha wanaendeleza nidhamu kazini pamoja na kufuata sheria na kanuni ziliopo ili kuwa wafanyakazi bora pamoja na kuleta maendeleo nchini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**DEREVA NA MAUZO**, KATIKA KAMPUNI YA MAJI NAFASI 8 0767 - 269677.


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Nipashe MWANGA WA JAMII

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0782253676


## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO.**

Usimamizi wa mirathi No;298/2020
Ombi la **MARTHA JORAM MACHA**
,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu
**HAPPINESS JORAM MACHA.**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **20/10/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **06/10/2020.**

21594262

---

**COMPANY NO 139901**
**THE COMPANIES ACT, 2002**
**NOTICE OF VOLUNTARY WINDING UP NOTICE**

is hereby given to the General Public that by special resolution dated 30th September, **2020 GNS CONSTRUCTION COMPANY LTD,** resolved to wind up the company voluntarily.
**FURTHER NOTICE** is given that **GEOFREY MAUYA** was appointed Liquidator for the purpose of winding up the company.
**TAKE NOTICE** that all creditors of the company are hereby requested to furnish the liquidator with full details of their claims against the company at the address shown below within fourteen **(14) days** from the date of this notice.
Dated at Dar es salaam, this 30th day of **September, 2020.**

21594292

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA PROBATE AND
ADMINISTRATION CAUSE NO.52. 2020
In the matter of the Estate of the late
DENIS WILLIAM BENDERA
of Kikuyu North Area within Dodoma Region
And IN THE MATTER OF THE APPLICATION
FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY
MUSSA DENIS BENDERA
GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 163)
All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 15 Day of OCTOBER 2020.
Dated at Dodoma this 13th day of AUGUST 2020

21594272

---

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa tarehe **13/10/2020** kampuni ya **Chico (China Henan Internation Cooperation Group co. Ltd** itapitisha gari lenye namba za usajiri **T346 BDU / T888 BDT,** yenye escort no **T643 CVZ** likiwa halijabeba kitu kutoka **DODOMA** kuelekea **TABORA** kupitia ITIGI,

2. Gari hilo linavipimo vifuatavyo

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **20.00m** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.00m** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.5m** |

3. Njia itakayo tumika ni **DODOMA hadi TABORA** kupitia **ITIGI** *Gari itasafiri muda wa mchana tu kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jion*

***Tunaomba radhi kwa usumbufu***

115942202

---

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa tarehe 17/10/2020 Kampuni ya **Chico (China Henan International Cooperation Group Co. Ltd)** itasafirisha mzigo **XCMG XLZ 2103S,** wake wenye vipimo vikubwa kutoka **TABORA kuelekea DODOMA kupitia ITIGI,** gari hilo lenye namba za usajiri **T346 BDU / T888 BDT,** yenye escort no **T643 CVZ na T805 TDV**

2. Gari hilo linavipimo vifuatavyo

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **20.00m** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.2m** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.0m** |

3. Njia itakayo tumika ni **TABORA hadi DODOMA kupitia ITIGI** *Gari itasafiri muda wa mchana tu kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jion*

***Tunaomba radhi kwa usumbufu.***

215942301

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi No. 147/2020.**

**Ombi la AURELIA H. RUSISYE kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu GEOFREY JOHN HOMVYE**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe 03/11/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 12/10/2020.

115943002

---

**ROCKY BHIMJI MANDANI**
amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajiri
**T 205 AUS**
aina yake
**TOYOTA-PREMIO.**

Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote Cha polisi POLISI TAARIFA .
Rb namba
**KAG/MUL/RB/654777/2020**.

21594282

---

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO.**

Usimamizi wa mirathi No;225/2020
Ombi la
**JOSEPH LUCAS MAKUKULA**
Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu
**SAMWEL LUCAS YOHANA**.
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **15/10/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **14/09/2020.**

21594312

---


***Uza, Chenye Thamani Kubwa***
***Kwa Kutangaza Nasi***
***Kwa Bei Poa***
***Tupigie***
***0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HABARI PICHA



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakivushwa kutoka upande wa Kinondoni kwenda Magomeni, baada ya barabara ya Kawawa, eneo la Mkwajuni, kujaa maji ya mvua. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Basi la shule likiwa limezima katikati ya mafuriko katika barabara ya Shekilan-go, eneo la Bamaga, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Magari yakiwa kwenye foleni eneo la Mwenge, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha jijini Dar es Salaam jana na kusababisha mafuriko katika barabara ya New Bagamoyo. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Baadhi ya wakazi wa Kitunda Kivule, jijini Da es Salaam, wakipanda ngazi kuvuka upande wa pili wa Mto Kerezange, baada ya barabara ya muda kukatika kutokana na mvua kubwa iliyonyesha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Moja ya nyumba zilizokumbwa na mafuriko katika eneo la Mkwajuni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# KOEMAN ARIDHIKA NA KIKOSI BARCA




**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Donald Koeman, amesema anaamini wachezaji waliomo kwenye timu yake ni wazuri na ana furahi kuwa nao, licha ya kushindwa kusajili wale aliowahitaji.

Barca ilishindwa kufanya usajili wa wachezaji wapya kutokana klabu hiyo kuyumba kiuchumi kulikosababishwa na janga la virusi vya corona.

Barca imeachana na wachezaji wake wanne katika dirisha lililopita, Luis Suarez, Arthur, Ivan Rakitic na Arturo Vidal na ikawasainisha Miralem Pjanic, Sergino Dest na makinda Trincao, Pedri na Matheus Fernandes.

"Kikosi kipo sawa sawa na nina furaha kuwa na wachezaji hawa, tulijaribu kufanya maboresho katika baadhi ya maeneo, lakini kuna baadhi ya wachezaji hatukufanikiwa kuwapata," alisema akinukuliwa na AS.

Barcelona ilitangaza kuwa imepata hasara ya pauni milioni 87 na kupoteza mapato ya pauni milioni 184 kutokana na janga la corona.

Koeman alikuwa anahitaji zaidi saini ya winga wa Uholanzi na Olmpique Lyon, Memphis Depay, lakini dili lilifeli na badala yake ameamua kumtumia Ansu Fati ambaye ameonekana kuonyesha kiwango kikubwa na kuwa kipenzi cha mashabiki wa Barca.




# Ronaldo hazuiliki kabisa – Kulusevski

**LISBON,** Ureno

DEJAN Kulusevski amesisitiza Cristiano Ronaldo hazuiliki wakati nyota hao wa Juventus wakitarajia kupambana leo, Jumatano wakiwa timu mbili tofauti za mataifa yao, kwenye mchezo wa Ligi ya Mataifa ya UEFA kati ya Sweden na Ureno.

Ronaldo na Ureno watawakaribisha Kulusevski na Sweden hapa Lisbon kwenye mchezo huo wa Kundi la 3.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or, Ronaldo alifunga mara mbili wakati Ureno ikiifunga Sweden mabao 2-0 kwenye mchezo uliopigwa Septemba mwaka huu.

Nyota wa Sweden, Kulusevski – ambaye anacheza na Ronaldo kwa mabingwa wa Serie A, Juve – amezungumzia namna ambavyo itakavyokuwa ngumu kumzuia mfungaji huyo wa wakati wote wa Ureno.

"Hakuna mtu anayeweza kumzuia. Kama akiwa kwenye siku yake nzuri, anaamua mwenyewe kila kitu," alisema Kulusevski akiiambia Aftonbladet.

Ureno inaongoza Kundi lake la 3, dhidi ya Ufaransa kwa tofauti ya mabao – huku wote wakiwa na pointi saba baada ya mechi tatu, ambapo ilitoka sare ya bila kufungana jijini Paris, Jumapili.

# Rodrygo akataa daraja la Neymar

**MADRID,** Hispania

NYOTA mkali wa Brazil, Rodrygo amesema hataki kuwa "Neymar mpya" wakati akielezea kufananishwa kwake na nyota mwenzake huyo.

Rodrygo ni mmoja wa wachezaji vijana wenye kipaji cha kuvutia akiwa anacheza soka lake pale kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Real Madrid.

Kinda huyo mwenye umri wa miaka 19, alinunuliwa kwa euro milioni 45 kutoka Santos na kujiunga na Madrid mwaka 2019, amekuwa akilinganishwa na nyota wa Paris Saint-Germain, Neymar na Robinho, ambao wote walitokea kwenye klabu hiyo ya Brazil.

Lakini Rodrygo hafurahii ulinganisho huo, akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa Brazil wa kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Peru jana Jumanne: "Tangu mwanzo kabisa nikianza kucheza Santos, walikuwa wananiita mimi kama 'Neymar mpya' na Robinho, nilikuwa sipendezwi kwa hilo.

"Mara zote nilikuwa nasema nataka kuwa Rodrygo na kutengeneza historia yangu, Robinho na Neymar ni wachezaji wakubwa wa Santos na wameshamaliza kazi yao pale.

"Nataka watu watambue kwamba, kuna Neymar mmoja tu. Sipendi kufananishwa naye, mimi nataka kuwa Rodrygo basi."

Rodrygo ambaye amecheza mechi tatu za kimataifa Brazil, ameshacheza mechi mbili za LaLiga kwa Madrid msimu huu wa 2020-21, akiwa amecheza mechi 19 msimu uliopita na mechi 26 kwenye mashindano yote.



HABARI MICHEZO

# Havertz: Ligi Kuu England ni ngumu

**LONDON,** England

KIUNGO wa Chelsea, Kai Havertz, amesema Ligi Kuu England ni ngumu na ya kutumia nguvu zaidi ikilinganishwa na ile ya Ujerumani, Bundesliga.


Nyota huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye alijiunga na Chelsea katika dirisha lililopita la majira ya joto kutoka Bayer Leverkusen, amecheza mechi tano chini ya kocha Frank Lampard.

"Ligi ya England ni tofauti kabisa na Bundesliga ambayo aina ya uchezaji wa timu zao ni za taratibu ukilinganisha na England ambazo zinahitaji mchezaji awe na nguvu na kasi sana," alisema akinukuliwa na gazeti la Bild.

Havertz alionekana kuwa kwenye kiwango kibovu katika mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu dhidi ya Brighton, lakini katika mchezo wa pili dhidi ya Barnsley alifunga 'hat-trick' kwenye ushindi wa mabao 6-0 katika michuano ya Kombe la Carabao.

Mchezaji huyo amesema anahitaji kupata muda mrefu zaidi wa kuzoea mazingira na aina ya soka la England ili kuonyesha kiwango ambacho mashabiki wengi wa Chelsea wanakitarajia kutoka kwake.

"Nimeanza kwa kiwango cha chini kwa sababu ligi hii ni tofauti kabisa na ile niliyotoka," alisema.




# DE BRUYNE ATOA SABABU KUMKATAA MESSI MAN CITY




**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester City, Kevin De Bruyne amesema klabu yake ina wachezaji wengi na wenye ubora, hivyo kusajiliwa ama kutosajiliwa kwa Lionel Messi hakumpi wasiwasi wowote.

Man City ilikuwa kwenye harakati za kuisaka saini ya mchezaji huyo wa Barcelona anayeshikilia rekodi ya kushinda tuzo za mchezaji bora wa dunia mara sita, katika dirisha lililopita.

Lakini dili hilo lilikwama baada ya Messi mwenyewe kukubali kubaki pale Barca kwa msimu mmoja zaidi.

"Sijali kuhusu hilo, kama atakuja litakuwa ni jambo jema na kama hatokuja ni jambo zuri pia, kwa sababu tuna wachezaji wazuri ambao najisikia furaha kucheza nao," alisema De Bruyne akinukuliwa na Sky Sport.

Uvumi umeenea kwamba, Messi anaweza kutua Man City katika dirisha lijalo la majira ya joto, hasa baada ya Ofisa Mtendaji wa klabu hiyo, Omar Berrada kunukuliwa akisema kuna uwezekano wa mchezaji huyo kusajiliwa katika kikosi chao.

"Ni miongoni mwa wachezaji wachache ambao wana vipaji vya kushangaza sana, pia anaweza kucheza kwenye klabu yoyote duniani na akaonyesha kiwango kikubwa pia," alisema Berrada.

"Huyu si mchezaji bora tu wa dunia kwa sasa, bali ni mchezaji bora wa kizazi chake.'

# *Southgate kumwanzisha Kane dhidi ya Denmark*

**LONDON,** England

GARETH Southgate ana matumaini mshambuliaji wake, Harry Kane atakuwa fiti kuanza kwa England wakati watakapocheza na Denmark kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa leo, Jumatano.

Kocha Mkuu wa Spurs, Jose Mourinho, alimwambia Southgate asimtumie Kane katika mechi zote tatu za mashindano hayo za England wakati huu wa mapumziko wa mechi za kimataifa, huku Tottenham wakiwa na mwanzo mzuri wa ligi msimu huu wa 2020-21.

Kane alifunga mara mbili wakati Spurs ilipoisambaratisha Manchester United kwa mabao 6-1 kwenye Ligi Kuu ya England, Oktoba 4, kabla ya kujiunga na timu ya Taifa ya England siku moja baadaye.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alionekana kuwa na maumivu ya nyama za paja na hakuwapo kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Wales Alhamisi iliyopita, na alianzia benchi katika mchezo dhidi ya Ubelgiji Jumapili kabla ya kuingia kuchukua nafasi ya Dominic Calvert-Lewin dakika ya 66.

Licha ya kauli hiyo ya Mourinho, Kocha wa England, Southgate anajiamini kwamba nahodha wake huyo atakuwa tayari kuanza dhidi ya Denmark leo, Jumatano.

"Kulikuwa na majadiliano na timu ya madaktari, kwa sababu hatutaki kuingia kwenye hatari, lakini naamini atakuwa fiti kucheza," alisema Southgate akiwaambia waandishi wa habari.

"Aliripoti Jumapili, na tulipata taarifa yake kuhusu maumivu yake, nina imani kubwa kuwa atakuwa fiti kucheza."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND MBADALA WA MBAPPE REAL MADRID

Kwa sasa miamba hiyo ya LaLiga inaona Mfaransa huyo anaweza kuwa biashara ngumu...

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid inamuona Erling Haaland kama ndiye chaguo lao la pili kama watashindwa kumsajili Kylian Mbappe kutoka klabu ya Paris Saint-Germain ya Ufaransa, kwa mujibu wa ukurasa wa mbele wa gazeti la Marca la jana, Jumanne.

**Mbappe kwa muda mrefu amekuwa akiwaniwa na kocha, Zinedine Zidane ili akakipige kule Real Madrid.**

Na mshambuliaji mwenyewe, Mbappe pia hajaficha siri namna gani anavutiwa na Mfaransa mwenzake huyo, Zidane.

Lakini suala la Mbappe kutua Real Madrid linaonekana kama linaweza kuwa gumu, kwani PSG nao hawataki kumuchia nyota huyo ambaye amekuwa na kiwango cha kuvutia.

Na sasa kwa kuwa Real Madrid wanaona Mbappe anaweza kuwa biashara ngumu kwao, wanamtolea macho Haaland na anaweza kupatikana kwa bei nafuu zaidi hasa kutokana na kipindi hiki cha mlipuko wa virusi vya corona.

Mshambuliaji huyo wa Borussia Dortmund, Haaland ambaye alitua huko Bundesliga Januari mwaka huu, sasa ndiye chaguo namba moja kwa Madrid kama wakimkosa Mbappe.

"Ni wazi kwamba usajili wa Mbappe kwenda Santiago Bernabeu unaweza kuwa mgumu, hivyo Madrid lazima waangalia chaguo jingine," liliandika gazeti la Marca.

"Chaguo hili si jingine bali ni Haaland, kwani anaweza kupatikana kwa bei nafuu zaidi."

Mbappe pia amekuwa akihusishwa na kuwaniwa na Liverpool, huku PSG wakionyesha wazi kabisa kutokuwa na mpango wa kumuachia nyota huyo ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2021.

## ZISIKUPITE

### UNITED KUMSAJILI CAMAVINGA

MANCHESTER United imeweka mipango ya kumsainisha kiungo wa Rennes na Ufaransa, Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 17, iwapo Mfaransa mwenzie Paul Pogba mwenye miaka 27, ataamua kuondoka Old Trafford. ***(Sport Witness)***

### DILI LA BENRAHMA KUKWAMA

UHAMISHO wa mshambuliaji wa Algeria, Said Benrahma mwenye umri wa miaka 25, wa thamani ya pauni milioni 25 kutoka Brentford kwenda West Ham uko hatarini kutofanikisha, ambapo wagonga nyundo hao wamejielekeza zaidi kwa mshambuliaji wa Bournemouth raia wa Norway, Josh King mwenye umri wa miaka 28. ***(Mirror)***

### MAN CITY WARUDIA TAGLIAFICO

KLABU ya Manchester City itajaribu tena kumsajili mlinzi wa kushoto wa Ajax na Argentina, Nicolas Tagliafico mwenye umri wa miaka 28, wakati wa dirisha la Januari. ***(Sun)***

### SPURS WAKOMAA NA MILAN

TOTTENHAM Hotspur huenda ikarejesha nia yake ya kumsajili mlinzi wa kati wa Inter Milan na Slovakia, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 25, Januari mwakani. ***(Team Talk)***

### FULHAM YAMTAKA KONGOLO

FULHAM wako katika hatua nzuri ya mazungumzo ya kumsajili mlinzi wa Huddersfield na Uholanzi, Terence Kongolo mwenye umri wa miaka 26. ***(Football Insider)***

### ROMERO ATIA HURUMA UTD

WACHEZAJI kadhaa wa Manchester United wameeleza masikitiko yao ya namna hali inavyomwendea mlinda mlango wa timu hiyo, Sergio Romero mwenye umri wa miaka 33, ambaye amekosa nafasi pale Old Trafford baada ya kurejea kwa Dean Henderson, lakini uhamisho wake wa siku ya mwisho ulishindikana kutokana na ada iliyowekwa ya pauni milioni 10. ***(ESPN)***

### BABA WA PARTEY ATOA SIRI

BABA mzazi wa kiungo mpya wa Arsenal na Ghana, Thomas Partey, amesema kwamba mtoto wake alikuwa anasubiri timu kubwa imfuate licha ya Juventus na Chelsea kuonyesha nia ya kumtaka kumsajili. ***(Mirror)***

### OZIL AVUNA FEDHA ARSENAL

KIUNGO wa zamani wa kimataifa wa Ujerumani anayeichezea Arsenal, Mesut Ozil, mwenye umri wa miaka 31, ambaye hajacheza kikosi cha kwanza tangu Machi mwishoni hadi sasa, atalipwa marupurupu ya mrahaba yanayofikia pauni milioni nane. ***(The Athletic - subscription required)***

### GUILBERT KUWANIA NAMBA

MLINZI wa Ufaransa, Frederic Guilbert, 25, ameapa kupambania nafasi yake ndani ya Aston Villa baada ya uhamisho wake kuelekea Nantes kukwama kwenye dirisha la usajili la majira ya joto. ***(Express and Star)***

### DEMBELE KIKWAZO KWA DEPAY

MPANGO wa Barcelona kutaka kumsajili nyota wa Lyon na timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 26, ulishindikana baada ya Ousmane Dembele mwenye miaka 23, kukataa kwenda Manchester United. ***(AS)***

HABARI MICHEZO

## Mtibwa na jambo lao kwa Gwambina

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema hawatoidharau Gwambina FC kwa sababu imepanda Ligi Kuu msimu huu, badala yake wanaingia kwa nguvu zote kesho kama wanacheza na timu yenye uzoefu ili kupata pointi tatu muhimu.

Kocha huyo amesema kuwa kutokana na ligi jinsi ilivyo kwa sasa, timu zote zilizopanda na zilizokuwa kwenye Ligi Kuu msimu uliopita, zina viwango vinavyofanana hivyo, haitakiwi kudharau mechi yoyote ile.

Mtibwa ambayo kesho itakuwa ugenini kucheza dhidi ya wenyeji Gambina kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza inashika nafasi ya 11 mpaka sasa kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi tano, ilizozipata baada ya kushinda mechi moja, sare mbili na kupoteza mechi mbili kwa mechi tano ilizocheza, huku wenyeji wao, Gwambina wakiwa kwenye nafasi ya 14 wakiwa na pointi nne, na kwenye mechi tano walizocheza wameshinda moja, sare moja na kufungwa tatu.

## TFF yaunda Kamati ya ushindi T/ Stars

**Na Mwandishi Wetu**

BOSI wa Kampuni ya GSM, Ghalib Said Mohamed, ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ushindi ya timu ya Taifa, 'Taifa Stars'.

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) iliyotolewa jana, ilieleza kuwa Rais wa shirikisho hilo, Wallace Karia, ameunda kamati hiyo ambayo Makamu Mwenyekiti wake ni Salim Abdallah 'Try Again' na Katibu wake akiwa Mhandisi Hersi Said ambaye ni Mkurugenzi wa Uendeshaji wa GSM.

Wajumbe wa kamati hiyo ni Abdallah Bin Kleb, Anita Rwehumbiza, Beatrice Singano, Christine Manyenye, Farid Nahdi na Feisal Abri.

Wengine ni Farough Baghozah, Haji Manara, Jerry Muro, Mohamed Nassor, Nandi Mwiyombella, Patrick Kahemele na Philemon Ntahilaja.

# SIMBA YATABIRIWA KUFIKA FAINALI MABINGWA AFRIKA

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa zamani wa Simba, Shekhan Rashid, amekitazama kikosi cha sasa cha timu hiyo na kuchambua uwezo wa mchezaji mmoja mmoja na uchezaji wao kitimu, kisha kutoka na utabiri kwa kueleza "ina uwezo wa kufika hatua ya fainali Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Shekhan, aliyeichezea Simba kwa miaka kadhaa kuanzia mwaka 2001, kabla ya kujiunga na Azam FC katikati ya mwishoni mwa miaka ya 2000, alisema anafurahia mno soka linalochezwa na Simba kwa sasa na kumkumbusha enzi zao hususan mwaka 1993 walipofika fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, CAF.

"Hii sasa ninayoiona ndiyo Simba. Ndiyo Simba ile yetu na ile ya mwaka 1993, na pia ile ya mwaka 2003 iliyocheza Ligi ya Mabingwa Afrika. Mwenyewe nikikaa nikiiangalia Simba ikicheza soka nafarijika sana," alisema.

**Shekhan, ambaye ni mchezaji za zamani wa Singida United, Moro United, Azam FC, pia akiwa amecheza soka la kulipwa nchini Sweden, alisema uwezo wa Simba kwa sasa unaweza kabisa kuifanya timu hiyo kufika hatua ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kama wakiwa makini.**

"Mpira kwa sasa si kama enzi zile. Soka limebadilika kabisa Afrika. Timu zinashinda kutokana na uwezo uwanjani na kujipanga, si figisu kama zamani kwa baadhi ya mechi, kwa ninavyoiangalia timu hii kama wakiwa makini wana kikosi kabisa cha kufika fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema.

Kuhusu mapungufu, alisema kuwa ni kweli pamoja na uwezo mkubwa lakini kikosi kina mapungufu kadhaa, ingawa uwezo wao ni mkubwa kuliko mapungufu waliyonayo.

"Mapungufu yapo, na hayakosekani, ila kikosi cha Simba kwa sasa kina uwezo mkubwa kuliko kasoro au mapungufu machache waliyokuwa nayo, kwa hiyo viongozi na makocha wanatakiwa kujipanga tu kwenye mechi za kimataifa, nina imani itafanya vizuri."

Shekhan, aliyekuwa kiungo mchezeshaji mwenye uwezo wa hali ya juu wa kuchezea mpira, aliisaidia Simba kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara msimu wa 2001/02, Kombe la FAT, Kombe la Tusker ambalo ilitwaa nchini Kenya na Kombe la Kagame.



Beki Mghana, Daniel Amoah (kulia), akimpongeza mshambuliaji Mzimbabwe Prince Dube baada ya kufunga mabao mawili dakika ya 44 kwa penalti na 45 katika ushindi wa 4-0 iliyoupata Azam FC juzi, dhidi ya Fountain Gate ya Daraja la Kwanza. Mabao mengine kwenye mchezo huo wa kirafiki uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, yalifungwa na kiungo Mudathir Yahya dakika ya 25 na Isamil Aziz Kada dakika ya 50. **MPIGAPICHA WETU**

# *Yanga yaianika Mwadui kwa Azam*

**Saada Akida na Adam Nyangasa,** TUDARCo

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Mromania Aristica Cioaba, amesema ameuona ubora na udhaifu wa uwanjani wa wapinzani wao, Mwadui FC kupitia Yanga, na kubaini timu hiyo haitaweza kuharibu mipango yao ya kutafuta pointi tatu katika dimba lao la nyumbani pale Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Cioaba alisema kikosi chake kipo fiti kwa ajili ya kuendelea pale kilipoishia ili kuhakikisha kinapata matokeo chanya katika mechi hiyo itakayopigwa kesho, Alhamisi.

Alisema ameiona Mwadui ikicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Yanga, na kwamba inacheza vizuri, lakini ameyasoma madhaifu yao, hivyo watayatumia kupata matokeo chanya na kuhakikisha mipango yao ya kuendelea kuganda kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo haisimamishwi.

"Nawaheshimu sana wapinzani wangu, waliisumbua Yanga katika mechi ya kirafiki, kwa upande wa kikosi changu nimekiimarisha kupambana kupata matokeo mazuri katika mechi zetu zote za ligi ikiwamo Mwadui," alisema Cioaba.

Naye kinara wa mabao wa Azam, Prince Dube, alisema anataka kuwa bora zaidi na kuisaidia timu hiyo kufanya vizuri katika mechi zake za ligi na michuano mingine msimu huu.

Alisema anahitaji kuona timu yake inafikia malengo waliyojiwekea hali ambayo inawafanya wapambane kupata matokeo mazuri katika kila mechi ikiwamo dhidi ya Mwadui.

"Nataka kusaidia timu yangu kupata matokeo mazuri katika kila mechi, kikubwa nataka kuwa bora zaidi kwa timu, tushinde mechi zetu kama timu na pia tuendelee kufanya vizuri zaidi katika mechi zinazokuja," alisema Dube.

Juzi, Azam FC iliibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya timu ya Daraja la Kwanza, Fountain Gate kwenye mchezo wa kirafiki uliochezwa Uwanja wa Azam Complex.

Bao la kwanza kwa Azam FC lilipachikwa na kiungo Mudathir Yahya dakika ya 24, huku Dube akitupia mawili dakika ya 44 na 45 wakati la nne likizamishwa nyavuni na Isamil Aziz Kada dakika ya 50.

Lakini wakati Cioaba akieleza hayo, Kocha Mkuu wa Mwadui FC, Khalid Adam, yeye amesema maandalizi ya kikosi chake yanaendelea vizuri na malengo yake ni kuhakikisha anaisimamisha timu hiyo iliyopo kileleni ikiwa na alama 15 baada ya kushinda mechi zote tano ilizocheza hadi sasa.

Akizungumza na gazeti hili jana kocha huyo alisema maandalizi yanaendelea vizuri japo kuna changamoto mbalimbali za hali ya hewa ambazo zinakwamisha baadhi ya vipindi vya mazoezi, ila wachezaji wote wana ari na mchezo huo.

"Azam ni timu nzuri sana na pia imeonyesha kiwango kizuri kwenye ligi na mpaka sasa haijapoteza mchezo, lakini mimi na vijana wangu tumejiandaa vizuri na tutapambana kuhakikisha tunaondoka na alama tatu muhimu katika mchezo huo na matokeo tutakayopata ni ya kimpira," alisema Khalid.

# Michezo

Jumatano Oktoba 14, 2020

Nipashe




Haaland mbadala wa Mbappe Real UKURASA 22

MUUAJI STARS...



Usajili mpya wa Yanga, straika Saidi Ntibazonkiza ambaye aliifunga Taifa Stars, Burundi ikishinda 1-0, akiwa na Mkurugenzi wa Kampuni ya GSM ambao ni wadhamini wa Klabu hiyo, Mhandisi Hersi Said (kulia), baada ya kusaini mkataba juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Morrison bado pasua kichwa TFF

**Saada Akida na Adam Nyangasa,** TUDARCo

SAKATA la kiungo wa Simba, Bernard Morrison bado limeendelea kuipasua kichwa Kamati ya Maadili ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), baada ya Mwenyekiti wa kamati hiyo, Wakili Kichere Mwita kueleza, limeshindwa kusikilizwa kwa kuwa mchezaji huyo alituma wawakilishi badala ya yeye mwenyewe kufika.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Wakili Mwita, alisema yapo mambo ambayo yanapaswa kuwakilishwa, lakini kwenye suala la Morrison ambalo ni la kimaadili alipaswa awepo yeye mwenyewe ili kujibu maswali mengine ambayo hayawezi kujibiwa na wawakilishi.

"Mashtaka dhidi ya Bernard Morrison kifupi ni kwamba mlalamikiwa hakufika mwenyewe alitoa udhuru, hiyo ndiyo sababu iliyofanya kamati kushindwa kutoa hukumu kwa kuwa alisema yupo na Klabu ya Simba.

"Alituma wawakilishi wawili, wanasheria ambao hata hivyo, kamati iliona kwamba ni haki mlalamikiwa mwenyewe awepo, hivyo iliamua kuahirisha suala hilo," alisema.

Aidha, alifafanua: "Kamati iliarifiwa kwamba suala la Morrison limeripotiwa Mahakama ya Usuluhishi ya masuala ya Michezo (CAS), lakini ieleweke pia iliyokatiwa rufaa ni kwenye masuala ya uamuzi ya usajili kamati ya usajili.

Kupitia kwa Makamu Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Frederick Mwakalebela, alidai kufikisha malalamiko TFF kuwa mkataba wa Simba na Morrison una dosari kutokana na kutosainiwa na kiongozi yeyote wa klabu hiyo, lakini sasa kamati hiyo imesema suala hilo wanaiachia CAS ambayo tayari Yanga ilishawasilisha malalamiko yao awali.

# NTIBAZONKIZA WA YANGA ASHTUA REKODI ZA MABAO

### Kacheza pia Uefa Cup, huku akiivaa Ajax na Feyenoord Ligi Kuu Uholanzi, lakini...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Klabu ya Yanga ikianza kujiimarisha mapema kuelekea dirisha dogo la usajili kwa kumpa mkataba wa awali nyota wa timu ya Taifa ya Burundi, Saidi Ntibazonkiza, rekodi za kucheka na nyavu za mshambuliaji huyo zinaonekana kushtua, imefahamika.

**Yanga juzi iliingia mkataba wa mwaka mmoja na nusu na mshambuliaji huyo ambaye aliizamisha Taifa Stars katika dakika ya 84 wakati Burundi ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 kwenye mechi ya kimataifa ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam Jumapili.**

Akizungumzia usajili huo, Mkurugenzi wa Kampuni ya GSM ambao ni wadhamini wa Klabu ya Yanga, Mhandisi Hersi Said, alisema tayari wamemsajili mchezaji huyo, lakini wataanza kumtumia kuanzia Desemba mwaka huu baada ya kukamilisha taratibu zote wakati wa usajili wa dirisha dogo Ligi Kuu Bara litakapofunguliwa Novemba mwaka huu.

Hersi alisema hawana wasiwasi kuhusu ubora wa mchezaji huyo kwa kuwa wamefuatilia kwa muda mrefu kabla ya juzi kufanikiwa kumpata na kuingia naye mkataba.

"Tulimfuatilia kwa muda mrefu na ni mchezaji aliyecheza klabu nyingi kubwa, hivyo tunatarajia ataisaidia timu yetu kufanya vizuri atakapoanza kuitumikia Desemba mwaka huu," alisema.

Kuhusu mpango wao wa kusajili vijana, lakini sasa wakiangukia kwa Ntibazonkiza mwenye umri wa miaka 33, Hersi alisema usajili huo ni pendekezo la kocha na wameangalia uzoefu zaidi na uwezo wake mkubwa, lakini pia ndicho kilichowafanya kumpa mkataba mfupi wa mwaka mmoja na nusu.

#### REKODI HAZIONGOPI

Hata hivyo, pamoja na Hersi kusifu uwezo wake, ukweli ni kwamba rekodi za Ntibazonkiza si za kutisha akiwa mbele ya lango, kwani katika klabu nyingi alizozichezea si mwenye kutisha kwa kutupia mabao.

Ntibazonkiza ambaye katika soka la ushindani alianzia Vital'O akiichezea kati mwaka 2003-2005, hiyo ndiyo timu pekee ambayo alifunga mabao mengi (70), lakini katika takwimu hizo zikiwa hazionyeshi idadi ya mechi alizocheza na kufunga mabao hayo.

Mwaka 2006-2010, aliichezea NEC Nijmegen ya Uholanzi jumla ya mechi 70 akifunga mabao nane pekee kabla ya 2010-2014 kujiunga na Cracovia ya Poland akiichezea mechi 85 na kucheka na nyavu mara 17, kisha mwaka 2014-2015 akajiunga na Akhisar Belediyespor ya Uturuki na katika mechi 13 alizocheza aliambulia kufumba bao moja tu.

Mwaka 2015-2016 alijiunga na Caen ya Ufaransa na kupata nafasi ya kucheza mechi 14 akifunga bao moja tu na kisha mwaka 2017 akatimkia Kaysar Kyzylorda ya Kazakhstan ambapo aliichezea mechi 10 akifunga mabao mawili pekee.

Hajaonekana tena dimbani kwa kipindi chote hicho sababu zikielezwa ni kutokana na kusumbuliwa na majeraha kwa kipindi kirefu, hadi mwaka huu alipoibukia Vital'O kujiweka fiti.

#### KACHEZA UEFA, NA DHIDI YA AJAX

Sifa nyingine kubwa ya Ntibazonkiza, ni mchezaji mwenye uzoefu wa kucheza mechi kubwa, kwani akiwa NEC Nijmegen alicheza Ligi Kuu ya Uholanzi dhidi ya Ajax Amsterdam na Feyenoord Rotterdam na timu nyingine maarufu kwenye ligi hiyo.

Lakini pia alicheza UEFA Cup dhidi ya FC Dinamo Bucuresti wakati akiitumikia NEC Nijmegen.

#### CHAGUO LA KOCHA

Wakati Kocha Mkuu wa Yanga, Mrundi Cedric Kaze akitarajiwa kutua leo usiku, imeelezwa Ntibazonkiza ni chaguo la kocha huyo na ndiye aliyependekeza asajiliwe.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002